# Daftari la Utetezi wa Imani kwa Wachungaji na Watumishi wa Kikristo

**Pima** kabla **hujaamini!**

1 Wathesalonike 5:21–22

AC/FAR
Africa Centre for Apologetics Research

Kumbuka Hatua Tatu

PIMA
Kila Kitu

ZINGATIA
kilicho Chema

EPUKA
Kila Aina ya Uovu

# Kuhusu "The Africa Centre for Apologetics Research"

(ACFAR, au Kituo cha Uchunguzi wa Utetezi wa Imani Afrika)

Dhamana ya ACFAR imejengwa katika Agizo Kuu la Yesu katika Mathayo 28, akituagiza kufanya mataifa yote yawe wanafunzi wake. Uanafunzi wa kibiblia unahusu kuwakuza waumini wapate kukomaa kiroho na kuwa na umoja, na katika hili, lazima tuufuate mfano wa mitume.

AC|FAR Africa Centre for Apologetics Research

## Msisitizo wetu ni wenye sehemu tatu:

Kwanza, tumepewa jukumu la kuwatayarisha watu wa Mungu wawe na ***uwezo wa kupambanua***, yaani, kuwasaidia kutofautisha kimaandiko kati ya ukweli na uongo, wema na ubaya, mwanga na giza. Tunajitahidi kuwapa uwezo wa kutambua utofauti wa dhati "kati ya kilicho sahihi na kinachokaribia kuwa sahihi," utofauti ambao makanisa ya uongo na walimu wa uongo huutumia. Makanisa na walimu bandia hustawi pasipokuwepo watu "waliokomaa, waliofunzwa kwa vitendo kubainisha mema na mabaya" (Waebrania 5:14).




Pili, tunalenga kuwafundisha waumini kwa ajili ya ***ulinzi wa imani*** "waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu" (Yuda 3–4). Agizo hili linatulazimu sisi kuishindania imani kwa nguvu katika uso wa upinzani. Si kwa silaha za kibinadamu za kuangamiza, bali kwa kiasi, kwa ukweli, kwa unyenyekevu tunapaswa kusema ukweli ambao Mungu amefunua kwa Roho wake katika Maandiko Matakatifu. Tito 1 hasa inawalazimu wachungaji, ambao ni mstari wa mbele wa ulinzi dhidi ya uongo, washike "kikamilifu ujumbe ule wa kuaminika kama unavyofundishwa. Ndivyo watakavyoweza kuwatia wengine moyo kwa mafundisho sahihi na kuyafichua makosa ya wale wanaopinga mafundisho hayo."

Tatu, tunalenga kuwahamasisha Wakristo wapate ***kufanya uinjilisti kati ya wale waliodanganywa na makanisa ya uongo,*** jukumu ambalo ni muhimu lakini limezembewa. Ina maana kwamba kuwasaidia kwa upendo wanaume, wanawake, na watoto walionaswa katika makanisa ya uongo, wamwamini Yesu Kristo kama Mungu hai na wa kweli, na kushika tumaini ambalo yeye tu anaweza kuwapa.

## Siku hizi, Wakristo wanalengwa na makanisa na walimu wa uongo wanaokusudia kuwadanganya, kuwapotosha, na kuharibu imani yao.

Waumini wengi sana, hata wachungaji, hawajatayarishwa kupambana na hili. ACFAR inawafundisha wachungaji na watumishi wengine wa Kristo kufahamu na kutumia ukweli wa kibiblia ili waweze kuwajibika ipasavyo dhidi ya mkanganyiko wa kiroho na upinzani unaotuzunguka.



Kwa neema ya Mungu, tunafanya kazi hii kupitia uchunguzi kuhusu makanisa ya uongo, kupitia huduma ya redio, na kwa kuandika na kusambaza maarifa kwa machapisho na kwenye mtandao kuikabili kiu iliyoenea ya kupata majibu. Kazi hii inawezeshwa kwa ushirikiano na makanisa, huduma zingine za kikristo zenye mtazamo mmoja, na watu waaminifu.

Tunatumaini kwamba utaomba pamoja nasi na pia kwa ajili yetu, na kutuunga mkono tukilenga kutimiza mwito wa Agizo Kuu kwa kuwafanya watu wawe wanafunzi wa Yesu na si wanaojiita wakristo tu, na hivyo wawe wakristo wenye ujasiri na uwezo wa kupima kila kitu, kuzingatia kilicho chema, na kuepuka kila aina ya uovu (1 Wathesalonike 5:21–22).

# Wewe na Utetezi wa Imani

Katika kiingereza neno *apologetics* (au, utetezi wa imani) limetoholewa kutoka neno la Kigriki *apologia* (au, ulinzi). Utetezi wa imani, kazi inayokazia ulinzi wa Ukristo, ni jukumu ambalo linaonekana kupotea katika kanisa la sasa. Siku hizi msisitizo mkubwa unaonekana kuwa kitu kama hiki, “Mungu ni Mungu wa upendo. Hebu, tupendane. Tusikabiliane na imani za watu wengine, kwa sababu huo si upendo.” Lakini, tofauti na mawazo kama haya, Yesu (ambaye ni kielelezo cha upendo) alikabili kwa nguvu imani za watu alizokutana nazo (k.m. Mathayo 23). Lazima sisi tuufuate mfano wake.

Utetezi wa Imani
ἀπολογία
huthibitisha kwa nini tunaamini kile tunachoamini.

Maandiko yametupa sisi mifano ya kufanya utetezi wa imani. Mtume Paulo, kwa mfano, alifanya kazi ya mtetezi wa imani alipotoa sababu za kuamini kwa Wayahudi na kwa watu wa mataifa (Matendo 17:15–34; 18:4). Apolo ni mfano mwingine mzuri sana, kwani katika Akaya aliitetea imani kwa dhati, akiwashida wapotevu katika majadiliano ya hadharani na kuthibitisha kutoka kwenye Maandiko kwamba Yesu ni Kristo (Matendo 18:24–28).

Utetezi wa imani huwapa wapotevu sababu za msingi zinazowawezesha wachague Ukristo badala ya dini yoyote nyingine. Utetezi wa imani unaweza kutumika kumwonyesha mpotevu kwamba chaguzi za dini zote zingine kikweli si chaguzi sahihi, kwani ni za uongo. Utetezi wa imani unaweza kuondoa vikwazo vya kimawazo vizuiavyo wapotevu ili wapate kuipokea injili.

Utetezi wa imani si kwa ajili ya kuwathibitishia wapotevu tu, bali pia ni kuwapa Wakristo usalama wa kiroho. Waumini wanaweza kuwa na uhakika wa kwamba imani yao si bila msingi, bali ni uchaguzi wenye busara uliojengwa juu ya ukweli. Utetezi wa imani haubadili imani yetu, bali unaimarisha imani tuliyo nayo.

Haya yameandaliwa kutokana na *5-Minute Apologetics for Today* • copyright © 2010 na Ron Rhodes • Ilichapishwa na Harvest House Publishers, Eugene, OR 97402 USA • www.harvesthousepublishers.com • Haya yametumika kwa ruhusa ya mwandishi.




Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

# Dini Zote si Sawa

Watu wengine wanadai kwamba dini zote kwa ujumla ni sawa, na tofauti zilizopo ni ndogo sana. Ukweli ni kwamba tofauti zilizopo kati ya dini zote ni za msingi na si za juujuu tu.

Watu wengine husema kwamba dini zote zinafanana kwa sababu zote zinafundisha maadili. Ukweli ni kwamba dini zote zingine za dunia zinalenga kuwasaida watu wabaya wapate kuwa bora zaidi kwa kuchagua maadili ya kibinafsi yaliyo bora zaidi. Kwa upande mwingine, Ukristo huwaalika watu waliokufa kiroho kuwa hai kiroho (Yohane 3:5).



Hili linafanikishwa kupitia sadaka iliyo kifo cha Yesu (2 Wakorintho 5:21). Yesu alidai kwamba maneno yake yana kipaumbele kuliko mafundisho ya watu wote wengine. Alisema kwamba yeye ni njia ya pekee ya wokovu kwa binadamu (Yohane 14:6). Wale waliomfuata walithibitisha hili (Matendo 4:12; 1 Timotheo 2:5). Yesu pia alionya kuhusu watu wengine ambao wangedai Kristo tofauti (Mathayo 24:4–5).

> Mtu akidai kwamba dini zote ni sawa, anaonyesha kwamba hazielewi dini hizo.

Dini mbalimbali pia zinafundisha mitazamo tofauti kuhusu Mungu. Yesu alifundisha kuhusu Mungu aliye Utatu (Mathayo 28:19). Muhammad, mwasisi wa Uislamu, alifundisha kwamba yule Mungu mmoja si aliye Utatu. Dini ya kihindi inaamini miungu mingi ambayo ni sehemu ya mungu mmoja aitwaye Brahman ambaye hana utu (yaani ni "impersonal"). Ubudha unafundisha kwamba dhana kuhusu Mungu kweli haina maana. Kama dini moja ya hizi ni sahihi, zile zote zingine si sahihi. Kama Yesu alikuwa sahihi, kama wanavyoamini Wakristo, zote zingine si sahihi.

Haya yameandaliwa kutokana na *5-Minute Apologetics for Today* • copyright © 2010 na Ron Rhodes • Ilichapishwa na Harvest House Publishers, Eugene, OR 97402 USA • www.harvesthousepublishers.com • Haya yametumika kwa ruhusa ya mwandishi.

# Wakristo Wanaweza Kudanganywa

Ni muhimu kuutafuta ukweli, kujiuliza maswali, na kufikiri kwa kina kwa sababu Wakristo wanaweza kudanganywa, yaani, wanaweza kukubali mafundisho yasiyo sahihi.

Ezekieli 34:1–7 husema wazi kwamba wanakondoo wa Mungu wanaweza kudhulumiwa na kupotoshwa na wachungaji waovu. Aidha, Yesu aliwaonya wafuasi wake kuchukua tahadhari dhidi ya manabii wa uongo wanaoonekana kwa nje kuwa wema lakini kwa ndani ni hatari (Mathayo 7:15–16). Kwa nini Yesu aliwaonya wafuasi wake kama haiwezekani kudanganywa?

> Wakristo wasioimarishwa katika ukweli wa kibiblia ndio hasa walio hatarini kukubali mafundisho ya uongo. Kwa hiyo, wakristo wanahitaji kujijenga kabisa kiroho katika Maandiko kila siku.

Yesu pia alionya wafuasi wake, "Jihadharini msije mkadanganywa na mtu. Maana wengi watatokea



wakisema kila mmoja kwamba yeye ndiye Kristo nao watawapotosha watu wengi....Watatokea manabii wengi wa uongo watakaowapotosha watu wengi" (Mathayo 24:4, 11). Kwa nini Yesu anawaonya wafuasi wake kuhusu udanganyifu kama wasingeweza kudanganywa na, mwisho wake, kuuamini uongo?

Hali kadhalika, katika 2 Wakorintho 11:2–3, mtume Paulo aliwaonya Wakristo katika mji wa Korintho kuhusu uwezekano wa kuacha uaminifu wa kweli kwa Kristo na kupotoshwa na mafundisho ya uongo.

Katika Matendo 20:28–30, Paulo aliwaonya wazee katika Efeso kuwa macho na kuchukua tahadhari kuhusu kanisa, hasa dhidi ya walimu wa uongo wasemao "mambo ya uongo ili kuwapotosha watu na kuwafanya wawafuate wao tu" (Angalia pia Waefeso 4:14; 2 Timotheo 4:3–4).

Haya yameandaliwa kutokana na *5-Minute Apologetics for Today* • copyright © 2010 na Ron Rhodes • Ilichapishwa na Harvest House Publishers, Eugene, OR 97402 USA • www.harvesthousepublishers.com • Haya yametumika kwa ruhusa ya mwandishi.



Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA

www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

# Manabii na Walimu wa Uongo

Mara nyingi, Maandiko yanaonya dhidi ya manabii wa uongo na walimu wa uongo kwa sababu watu wa Mungu mwenyewe wanaweza kudanganywa (Ezekieli 34:1–7; Mathayo 7:15–16, 24:4, 11). Kwa hiyo, Biblia huwahimiza waumini kuwapima wale wanaojidai kuwa manabii (Angalia 1 Yohane 4:1–3).

**Kwa namna gani waumini wanaweza kumtambua nabii wa uongo? Fikiria mawazo haya ya msingi:**

- Manabii wa uongo wanatabiri kisichotimia. (Kumbukumbu 18:21–22).
- Manabii wa uongo nyakati zingine watawashawishi watu kufuata miungu ya uongo na sanamu (Kutoka 20:3–4; Kumbukumbu 13:1–3).
- Manabii wa uongo mara nyingi hukana uungu wa kweli wa Yesu Kristo (Wakolosai 2:8–9).

Tunapaswa kufuata mfano wa Waberea kwa kupima na Maandiko mafundisho yoyote yanayodaiwa kuwa kweli.
(Matendo 17:11; 1 Wathesalonike 5:21)



- Manabii wa uongo mara zingine watakana ubinadamu wa Yesu Kristo (1 Yohane 4:1–2).
- Manabii wa uongo mara zingine huagiza kuepukana na vyakula fulani kwa sababu za kiroho (1 Timotheo 4:3–4).
- Manabii wa uongo mara kwa mara huhimiza masharti mengi (Wakolosai 2:16–23).
- Manabii wa uongo mara zingine hufundisha kwamba ndoa ni kitu kibaya (1 Timotheo 4:3).
- Manabii wa uongo mara kwa mara hupendekeza aina mbalimbali za uzinzi (Yuda 4–7)

Kama mtu anayesemekana kuwa nabii akisema chochote ambacho kinapinga sehemu yoyote ya Neno la Mungu, mafundisho yake yasikubaliwe. Neno la Mungu ni kipimo cha ukweli, kipimo kinachobainisha uongo.

Haya yameandaliwa kutokana na *5-Minute Apologetics for Today* • copyright © 2010 na Ron Rhodes • Ilichapishwa na Harvest House Publishers, Eugene, OR 97402 USA • www.harvesthousepublishers.com • Haya yametumika kwa ruhusa ya mwandishi.



# Mafundisho ya Lazima ya Imani ya Kikristo



Mafundisho ya msingi ya Biblia yamekuwa ni kiini cha Ukristo kwa miaka 2,000. Kwa ujumla, Wakristo wote wanaotaka kuwa na imani iliyo ya kibiblia wanayakubali mafundisho haya. Labda Wakristo hawakubaliani kuhusu mafundisho madogo madogo katika imani, lakini wanapaswa kukubaliana kuhusu mafundisho makuu, kweli hizi zilizo kiini cha Ukristo.

**Tunaweza kutambua mafundisho ya kimsingi ya imani ya kikristo kwa kuchunguza ukweli wa Injili, ulio wokovu wa binadamu kupitia maisha, kifo, na ufufuo wa Yesu Kristo.** Wokovu, kama Mungu alivyokuwa ametufunulia katika Maandiko Matakatifu yake, unamaanisha kwamba msamaha wa dhambi na uhai wa milele na Mungu unapatikana kwa kukiri kwamba "Yesu ni Bwana" na kuamini kwamba Mungu alimfufua Yesu kutoka wafu (Waroma 10:9). Tukichunguza ujumbe wa Injili, tunaweza kutambua mafundisho kumi na nne (14) ambayo ni ya lazima ili kupata wokovu kuwezekane.

Mafundisho ya kimsingi ya Ukristo yahusu:

- Mungu ni nani
- Yesu Kristo ni nani
- Upendo wa Mungu kwa watu, na hamu yake kuwaokoa

*Haya ni mafundisho 14 ya kimsingi kuhusu wokovu ambayo lazima yawe ya kweli au mtu yeyote hawezi kumjua Mungu na kuokolewa:*

## 1 Umoja wa Mungu

Kuna Mungu mmoja tu aliye wa kweli. Tangu milele ya zamani yupo, na atakuwepo kwa milele ijayo. Kuna Mungu mmoja, mmoja tu, aliye Muumba wa vyote.

## 2 Utatu wa Mungu

Ingawa kuna Mungu mmoja tu, yupo tangu milele ya zamani akiwa na nafsi tatu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

## 3 Upotovu wa Binadamu Wote

Mungu anataka kujulikana na watu na kuwa na mahusiano na binadamu. "Upotovu wa binadamu wote" unamaanisha kwamba kila mtu ametengwa na Mungu kiroho, na hana uwezo kabisa wa kujiokoa.



ACFAR

Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA

www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

## 4 Kristo Kuzaliwa na Bikira

Yesu alizaliwa kwa njia ya ajabu, kwa njia ya muujiza wa Mungu: Maria, mama yake Yesu, alipata mimba bila kukutana na mume au kujuana kimwili.

## 5 Kristo Kutotenda Dhambi Kabisa

Kristo alizaliwa na bikira, hivyo ubinadamu wake haukuathiriwa na dhambi. Kwa maisha yake yote Yesu hakutenda dhambi.

## 6 Uungu wa Kristo

Kulikuwa na njia moja tu ya binadamu kupatanishwa kiroho na Mungu. Mungu, bila kuacha uungu wake kwa kiasi chochote, alijivika na ubinadamu wetu, akawa mtu mkamilifu katika Kristo. Kristo asingekuwa Mungu na binadamu kwa mara moja, asingeweza kuwa mpatanishi kati ya Mungu na binadamu (1 Timotheo 2:5).

## 7 Ubinadamu wa Kristo

Ingawa Yesu ni Mungu, pia yeye ni binadamu kabisa. Yesu aliwahi kuchoka; Alisinzia; Alitoa jasho; Aliwahi kuwa na kiu na njaa. Yesu asipokuwa binadamu asilimia mia, asingeweza kutoa malipo ya dhambi za binadamu. Alihitaji kuwa na uungu ili awe na uwezo wa kutuokoa, na alihitaji kuwa na ubinadamu ili apate kutuwakilisha sisi binadamu. Lazima Kristo awe Mungu na Binadamu.

## 8 Ulazima wa Neema ya Mungu

Kwa sababu ya upotovu wa binadamu, hatuwezi kujiokoa. Ni kwa njia ya neema ya Mungu tu kwamba wokovu unawezekana. Mungu ana haki ya kuwawajibisha binadamu kwa sababu ya dhambi zao. Lakini, kwa neema yake, watu wasiostahili watapata ushirikiano naye na kuepukana na hukumu. Bila neema ya Mungu, hakuna mtu yeyote ambaye angaliweza kuwa na uhusiano na Mungu.

## 9 Ulazima wa Imani

Imani ni kutegemea kwamba Mungu anaweza kutuokoa na atatuokoa. Hakuna mtu yeyote anayeweza kustahili wokovu. Hakuna kiasi chochote cha matendo mema ambacho kinaweza kumrudishia Mungu deni analodai. Lakini, kwa kumwamini Mungu na kwa kupokea kwa shukrani zawadi yake ya wokovu, tunaweza kupatana naye Mungu. Kuamini ni wajibu wetu, lakini si tendo linalotustahilisha. Kuamini ni kumtegemea Mungu afanye kile ambacho tusingeweza kukifanya wenyewe (Waefeso 2:8–9; Tito 3:5–6).

## 10 Kifo cha Kristo kuwa Malipo ya Dhambi

Hukumu ya dhambi ni kifo—na si kifo cha kimwili tu (kilicho utengano kati ya roho zetu na miili yetu), bali pia ni kifo cha kiroho (kilicho utengano kati yetu na Mungu). Malipo anayotudai Mungu yalilipwa na Kristo kupitia kifo chake msalabani. Malipo yaliyofaa yalihitaji kuwa makamilifu, bila kasoro au upungufu. Kristo, aliye mtu mkamilifu, alijitoa kwa niaba yetu, ili kwamba kila amwaminiye hatakufa (kimwili au kiroho) bali atakuwa na uhai wa milele (Yohane 3:16).

## 11 Ufufuo wa Kristo Kimwili

Kifo cha Yesu kilikuwa malipo ya dhambi zetu, lakini mchakato wa kutupatia wokovu haukuisha mpaka alipokishinda kifo kwa kufufuka kimwili katika mwili uleule (Yohane 2:19–21). Kwa sababu Kristo ni mshindi dhidi ya kifo na mwili wake ni mfano wa miili ya ufufuo, binadamu wote watafufuliwa na kuishi kwa milele mbinguni au kwenye ziwa la moto.

## 12 Kristo Kupaa Kimwili Kwenda Mbinguni

Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, akafufuka kimwili kwa ajili ya wokovu wetu. Baada ya siku arobaini, alipaa kimwili kwenda mbinguni.

## 13 Upatanisho wa Kristo

Kupaa kwa Kristo kimwili kulimwezesha awe mpatanishi wetu (au kuhani mkuu) mbele za Mungu. Mbele zake Mungu, Kristo hutuombea daima.

## 14 Ujio wa Pili wa Yesu

Kama vile alivyoondoka toka duniani kimwili, ndivyo atakavyorudi. Ujio wa pili wa Yesu ni tumaini la dunia. Atakaporudi, waumini wafu watapata miili yao ya ufufuo. Waumini walio hai atakaporudi, hawatakufa, bali miili yao itabadilishwa kuwa miili itakayodumu kwa milele. Ujio wa Kristo wa kimwili utaonekana kwa wote, na waumini watatawala pamoja naye katika ufalme wake na kuishi pamoja naye kwa milele. Wale wasioamini watatengana na wema wake Mungu milele.

## Kuamini au Kutoamini?

Si lazima mtu aelewe mafundisho haya yote wakati anapomwamini Yesu na kuokolewa. Kuna utofauti kati ya mafundisho yale ambayo ni lazima yawe kweli ili tuokolewe na mafundisho yale ambayo ni lazima tuamini ili tuokolewe. Kwa mfano, hakuna sehemu yoyote katika Biblia ambayo inasema ni lazima kuelewa kwamba Yesu alizaliwa na bikira ili kwenda mbinguni; hata hivyo, ukweli wa kwamba Yesu alizaliwa na bikira unatuhakikishia kwamba Mungu alifanya kazi katika kuvunja minyororo ya dhambi kupitia Mwanae Yesu.

Kuna mafundisho mengine ya lazima ambayo labda mtu hayajui wala hayaelewi moja kwa moja lakini bado ameokolewa (kama ukweli wa kwamba Yesu alizaliwa na bikira, alipaa kwenda mbinguni, na atarudi duniani tena). Kusema hivi si kuleta maana ya kwamba mtu anaweza kuyakana (akiyasikia) na bado kuokolewa, bali ni kusema hahitaji kuyaelewa moja kwa moja ili aokolewe. Aidha, kuna mafundisho mengine ya lazima ambayo ni lazima **kuyaelewa** hapohapo ili kuokolewa. Mtu lazima aamini kwamba Kristo alikufa kwa ajili yetu, akafufuka (Waroma 10:9; 1 Wakorintho 15:1–6). Mtu lazima aamini “katika Bwana Yesu Kristo” (Matendo 16:31). Neno “Bwana” (*kurios* katika Kigiriki) likimrejea Kristo katika Agano Jipya linamaanisha “aliye Mungu,” kwa hiyo mtu hawezi kukana uungu wa Kristo na kuokolewa (Matendo 2:21, 36; 3:14–16; 5:30–35; 10:39; 1 Wakorintho 12:3).

Haya yameandaliwa kutokana na *Essential Doctrine Made Easy* na Norman L. Geisler (Rose Publishing, 2007)



ACFAR

Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA

www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

# Mafundisho ya Kibiblia kuhusu Utatu

Mungu ni mmoja mkamilifu kabisa akiwa na asili moja na nafsi tatu. Asili yake ni vile alivyo katika uhusiano wake na ulimwengu, yaani, vitu vyote alivyoumba. Nafsi zake ni tatu, zikiwa zinahusiana kati yao.

Wakristo wanaposema kwamba wanamwamini Mungu mmoja katika nafsi tatu (yaani, Utatu), ***hawamaanishi*** kwamba:

Ni Mungu 1 katika miungu 3, au

Ni nafsi 3 katika nafsi moja, au

Ni nafsi 3 katika miungu mitatu, au

Ni nafsi 1 katika miungu mitatu.

Bali, wanamaanisha kwamba:

Ni Mungu mmoja katika nafsi tatu.

Kwa hiyo,

Baba ni Mungu—nafsi ya kwanza ya Utatu.

Mwana ni Mungu—nafsi ya pili ya Utatu.

Roho Mtakatifu ni Mungu—nafsi ya tatu ya Utatu.

## Kwa nini Wakristo wanauamini Utatu?

Biblia hufundisha wazi kwamba kuna Mungu mmoja tu, ingawa nafsi zote za Mungu zinaitwa Mungu.

**Kuna Mungu mmoja tu:**

- "Basi sikilizeni enyi Waisraeli! Mwenyezi-Mungu, Mungu wetu, ni Mwenyezi-Mungu mmoja." (Kumbukumbu 6:4)
- "Kabla yangu hajapata kuwapo mungu mwingine, wala hatakuwapo mungu mwingine." (Isaya 43:10; 44:6, 8; 45:5a)

**Baba ni Mungu:**

- "Nawatakieni neema na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu na Bwana wetu Yesu Kristo." (1 Korintho 1:3; 8:6; Waefeso 4:4–6)

**Mwana ni Mungu:**

- "Neno alikuwa Mungu." (Yohane 1:1–5, 14) Yesu anatambulika kama "Neno."
- "Mimi na Baba, tu mmoja." (Yohane 10:30–33)
- Tomasi, aliye mwanafunzi wa Yesu, alimwita Yesu, "Bwana wangu na Mungu wangu." (Yohane 20:28) Yesu hakumwambia Tomasi kwamba alikosea kwa kumwita hivyo, bali alikubali kukubali kuitwa hivyo. Wengine katika Maandiko (k.m. Paulo na Barnaba, Matendo 14), walikataa kuabudiwa kama miungu.
- "Lakini kuhusu Mwana, Mungu alisema: "Kiti chako cha enzi, ee Mungu, chadumu milele na milele! Wewe wawatawala watu wako kwa haki." (Waebrania 1:6–8).
- "Kwa sababu hiyo Mungu alimkweza juu kabisa, akampa jina lililo kuu kuliko majina yote. Ili kwa heshima ya jina la Yesu, viumbe vyote mbinguni, duniani na kuzimu vipige magoti mbele yake, na kila mtu akiri kwamba Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba." (Wafilipi 2:9–11)

Paulo, mwandishi wa barua kwa Wafilipi, alisema kuhusu Yesu kilichosemwa kuhusu Mwenyezi-Mungu katika Isaya 45:23, halafu akamaliza kwa kusema Yesu ni Bwana, yaani, ni Mwenyezi-

Mungu yuleyule wa Agano la Kale.

Angalia aya hizi kuhusu umungu wa Yesu: Isaya 7:14; Isaya 9:6; Yohane 1:1; Yohane 8:58, 59; Yohane 10:30; Matendo 20:28; Waroma 9:5, 10:9–13; Wakolosai 1:15, 16; Wakolosai 2:9; Tito 2:13; Waebrania 1:3, 8; 2 Petro 1:1; 1 Yohane 5:20.

## Roho Mtakatifu ni Mungu:

- "Basi, Petro akamwuliza, "Anania, mbona Shetani ameuingia moyo wako na kukufanya umdanganye Roho Mtakatifu. . . Hukumdanganya mtu; umemdanganya Mungu!" (Matendo 5:3–4) Mstari huu unamtambua Roho Mtakatifu kuwa Mungu.
- "Hapa Bwana ni Roho." (2 Wakorintho 3:17) Neno "Bwana" hapa lamrejea Mwenyezi-Mungu katika mstari wa Agano la Kale (Kutoka 34:34) ambao alinukuu katika mstari uliotangulia (2 Wakorintho 3:16).

## Zaidi ya mistari 60 ya Biblia hutaja nafsi tatu za Mungu pamoja:

- Mathayo 3:16–17 Mara tu Yesu alipokwisha batizwa, alitoka majini; na kumbe mbingu zikafunguka, akaona Roho wa Mungu akishuka kama njiwa na kutua juu yake. Sauti kutoka mbinguni ikasema, "'Huyu ndiye Mwanangu mpendwa, nimependezwa naye.'"
- Mathayo 28:19 "Nendeni basi, mkawafanye watu wa mataifa yote wawe wanafunzi wangu, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu . . ."
- 2 Wakorintho 13:14 "Neema ya Bwana Yesu Kristo na upendo wa Mungu na umoja wa Roho Mtakatifu, viwe nanyi nyote."
- Waefeso 4:4–6 "Kuna mwili mmoja na Roho mmoja, kama vile tumaini mliloitiwa na Mungu moja. Kuna Bwana mmoja, imani moja na ubatizo mmoja; kuna Mungu mmoja na Baba wa wote, afanya kazi katika yote na yuko katika yote."
- Tito 3:4–6 "Lakini wakati wema na upendo wa Mungu, Mwokozi wetu ulipofunuliwa, alituokoa si kwa sababu ya jambo lolote jema tulilotenda sisi, bali kwa sababu ya huruma yake, kwa njia ya Roho Mtakatifu anayetujalia tuzaliwe upya na kuwa na maisha mapya kwa kutuosha kwa maji. Mungu alitumiminia Roho Mtakatifu bila kipimo kwa njia ya Yesu Kristo..."

Angalia pia Yohane 3:34–35; Yohane 14:26; Yohane 15:26; Yohane 16:13–15; Waroma 14:17–18; Waroma 15:13–17; Waroma 15:30; 1 Wakorintho 6:11, 17–19; 1 Wakorintho 12:4–6; 2 Wakorintho 1:21, 22; 2 Wakorintho 3:4–6; Wagalatia 2:21–3:2; Wagalatia 4:6; Waefeso 2:18; Waefeso 3:11–17; Waefeso 5:18–20; Wakolosai 1:6–8; 1 Wathesalonike 1:1–5; 1 Wathesalonike 4:2, 8; 1 Wathesalonike 5:18–19; 2 Wathesalonike 3:5; Waebrania 9:14; 1 Petro 1:2; 1 Yohane 3:23–24; 1 Yohane 4:13–14; na Yuda 20–21.

Haya yameandaliwa kutokana na *The Trinity* (Rose Publishing, 1999)



AC|FAR
Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.
Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

# Aina Sita za Mafundisho ya Uongo

## Tabia za Mafundisho ya Makanisa ya Uongo

*Si kwamba makanisa yote ya uongo yanafanya makosa yaleyale, lakini kuna sehemu kadhaa katika imani yetu ambazo mara kwa mara zinachafuliwa na walimu wa uongo. Vipengele vifuatavyo vinadhihirisha sehemu sita za imani ambazo mara kwa mara zinapotoshwa na walimu wa uongo, na vinaonyesha mifano mifupi ya jinsi wanavyouharibu ukweli.*

1 **Ufunuo**—Mara nyingi, makanisa ya uongo yatumia mafundisho ambayo huyapindisha, huyakana, na huyaongezea Maandiko kwa njia inayowaelekeza watu mpaka kwenye maangamizi. Wanadai kwa uongo kuwa na mamlaka ya kiutume au kinabii. *Mifano:*

- **Umormoni** (Joseph Smith alijidai kuwa nabii; alitunga Kitabu cha Mormoni na "maandiko" mengine ya kimormoni.)
- **Mashahidi wa Yehova** (wadai kwamba Mungu huongea kupitia shirika la Mnara wa Mlinzi tu na kwamba ni watu wa "tabaka ya wapakwa mafuta" ambao wanaweza kufasiri Biblia.)
- **Kanisa la** Waadventista Wasabato (Humwona Ellen G. White kama nabii maalumu wa Mungu katika siku za mwisho.)

2 **Mungu**—Mara nyingi mafundisho yao husisitiza miungu ya uongo au kugeuza kwa hatari mafundisho kuhusu Mungu wa kweli yawe ya uongo. *Mifano*:

- **Umormoni** (Hudai kwamba kuna miungu mingi, kwamba Mungu Baba aliwahi kuwa mtu aliyetenda dhambi katika sayari nyingine, na kwamba sisi tunaweza kufanywa kuwa miungu kama alivyo Mungu Baba.)
- **Mashahidi wa Yehova** (Hudai kwamba Utatu wa Mungu ni uongo, wakisema kwamba Mungu Baba tu ni Mungu wa kweli.)
- **Wapentekosti wa Umoja wa Mungu Tu** (Hudai kwamba Utatu ni uongo, wakisema Yesu ni Baba, Mwana, *na* Roho Mtakatifu.)

3 **Kristo**—Mara nyingi makanisa ya uongo hukana kwamba Kristo ni Bwana, au ni binadamu, au ukweli wa kwamba yeye ni nani. *Mifano*:

- **Mashahidi wa Yehova** (Hudai kwamba Yesu Kristo alikuwa kwanza malaika Mikaeli, halafu akawa binadamu mkamilifu, na si Mungu-mwanadamu.)
- **Umormoni** (Hudai kwamba Yesu hakuzaliwa na bikira, kwa kuwa Mungu Baba alifanya tendo la ndoa na Maria ili Yesu apate mwili wa kibinadamu.)
- **Wakristadelfiani** (Hudai Yesu hakuwa Mungu. Alikuwa na asili ya dhambi, na alihitaji kujiokoa kwanza kabla hajaweza kumwokoa mtu yeyote mwingine.)

4 **Wokovu**—Makanisa ya Uongo mengi hufundisha kuokolewa kunapatikana kupitia kutii masharti mengi, au hudai wokovu ni nafasi ya kuridhisha tamaa zetu. Hukana maana ya injili ya kifo na ufufuo wa Yesu, nk. Mifano:

- **Umormoni** (Masharti yao ni pamoja na kujipatia wokovu kwa kuustahili kulingana na juhudi zetu na kuamini Joseph Smith ni nabii wa Mungu.)
- **Mashahidi wa Yehova** (Masharti yao ni pamoja na kutumikia katika shirika la Yehova lilio lake la kweli, yaani shirika la Mnara wa Mlinzi.)

5 **Kanisa**—Makanisa ya uongo hufanya juhudi za kuwatoa watu kutoka katika ushirikiano wa Wakristo wa kweli, mara nyingi hulikataa kabisa kanisa. *Mifano*:

- **Umormoni** (Hudai kwamba makanisa yote mengine ni ya uongo na kwamba mafundisho ya makanisa yote mengine ni chukizo kwa Mungu.)
- **Kanisa la Laodisia** (Hadai kwamba Wakristo wa kweli wote lazima watoke makanisa yao ili wamfuate William Branham, nabii wa kweli wa Mungu katika siku za mwisho.)

6 **Siku za Mwisho**—Makanisa ya uongo mara nyingi hujaribu kutabiri mambo ya mbeleni yakidai mamlaka kutoka kwa Mungu, kudai kuhusu kurudi kwake Kristo kulishatendeka, nk. Mifano:

- **Mashahidi wa Yehova** (Walikosea kwenye kutabiri siku ya kurudi kwa Yesu kuwa katika mwaka 1874 halafu tena katika mwaka 1914. Pia walikosea kwenye kutabiri vita vya Armagedoni (yaani vita ya mwisho wa dunia kabla ya kuja kwake Yesu) kuanza katika 1941 na 1975.

Haya yameandaliwa kutokana na study na Robert M. Bowman, Jr.

# Maonyo ya Maandiko dhidi ya Uchawi na Ushirikina

Katika Agano la Kale na Agano Jipya, Mungu huwaamuru watu wake kuepukana na uchawi na ushirikina, na huyatumia maneno makali. Kila wakati, Biblia huhusisha uchawi na ushirikina na tendo la kuabudu sanamu, udanganyifu, hofu, ubatili, unajisi, na uasi. Mungu huona mambo haya kuwa maovu, ya kishetani, na ya kustahili hukumu kali na ya haraka.

### Biblia Huhukumu Uganga na Uaguzi

Mwanzo 41:8, 24
Kutoka 7:11, 22; 8:7, 18–19
Walawi 19:26
Kumbukumbu 18:10
2 Wafalme 17:17; 21:6
2 Nyakati 33:6
Isaya 47:9, 12
Yeremia 27:9
Matendo 8:9–11, 18–21; 13:6–12; 19:19
Ufunuo 9:20, 21; 18:23, 21:8; 22:15

### Biblia Huhukumu Matumizi ya Hirizi

Isaya 3:18–20
Ezekieli 13:18–20

### Biblia Huhukumu Uchawi

Kutoka 22:18
Walawi 19:26
Kumbukumbu 18:10, 14
2 Wafalme 17:17, 21:6
2 Nyakati 33:6
Isaya 47:9
Yeremia 27:9–10
Mika 5:12
Nahumu 3:4
Matendo 8:9–11; 19:19
Wagalatia 5:19–21
Ufunuo 9:21, 18:23, 21:8, 22:15

### Biblia Huhukumu Kupigiwa Ramli au Kujaribu Kuwasiliana na Mizimu

Walawi 19:31, 20:6
Kumbukumbu 18:10–11
1 Samueli 28:3, 9
2 Wafalme 21:6, 23:24
1 Nyakati 10:13
1 Nyakati 33:6
Isaya 8:19, 19:3
Yeremia 27:9

### Biblia Huhukumu Kuloga

Kumbukumbu 18:9–11
Isaya 47:9, 12
Mika 5:12

### Biblia Huhukumu Kupiga Bao

Walawi 19:26
Kumbukumbu 18:10, 14
1 Samueli 15:23



ACFAR

Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

# Maonyo ya Maandiko dhidi ya Uchawi na Ushirikina

2 Wafalme 17:17, 21:6
2 Nyakati 33:6
Isaya 2:6
Yeremia 27:9–10
Matendo 16:16–20

**Biblia Huhukumu Ushirikina**

Kumbukumbu 18:10, 14
1 Samueli 15:23
2 Wafalme 21:6
2 Nyakati 33:6
Mika 5:12
Nahumu 3:3–4
Wagalatia 5:19–21

**Biblia Huhukumu Unajimu (Kubashiri kwa Kuangalia Nyota)**

Kwa kuwa unajimu ni namna ya kubashiri mambo yajayo, ni marufuku kufanya hivyo kulingana na aya kama Walawi 19:26. Pia tunaweza kujifunza zaidi tukiangalia mistari kama ifuatayo:

- Isaya 47:13–15 (hapo wanajimu walidharauliwa na kuhukumiwa)
- Yeremia 8:1, 2: 10:2 (wale wanaofuata jua, mwezi, na nyota, na kuviabudu, na kutafuta ushauri huhukumiwa.)
- Daniel sura ya 2, 4, 5 (Baada ya wanajimu na wapiga bao kudai kwamba kufasiri ndoto za Nebukadneza na maono ya Belshaza hakuwezekani, Danieli alivifasiri kwa msaada wa Mungu.)

Haya yameandaliwa kutokana na *Christianity, Cults, and the Occult* (Rose Publishing, 2006)



## Nini Kinachofanya Unajimu Ukubalike?

Mtetezi wa imani wa Kikristo aitwaye Vishal Mangalwadi, katika kitabu chake *Wisdom from India: Astrology* (*Hekima Kutoka Uhindi: Unajimu*), anaainisha sababu tatu kuu zinazofanya unajimu kuwavutia watu wengi siku hizi:

- Unajimu humpa mtu jibu la matatizo yake.
- Unajimu huondoa kujihisi kuwa na hatia na adhabu.
- Unajimu humpa mtu mwongozo wakati anapohisi kukata tamaa na kupoteza mwelekeo.

## Unajimu Unafanya Kazi Vipi?

Unajimu si tu kwamba unakatazwa kwenye Biblia, bali pia unajimu ni jambo la kishetani. Mwandishi mmoja wa kitabu kinachohusu unajimu, Charles Strohmer, *What Your Horoscope Doesn't Tell You*, ambaye pia aliwahi kuwa mnajimu mahiri, alieleza, "Wafuasi wa unajimu wanawasiliana—bila wao kujua—na watu wa kiroho wa udanganyifu wenye ufahamu fulani." Anaendelea kueleza kuwa wanatumia jedwali au chati ya kinajimu kama chombo cha kuwasiliana na hizo roho kwa ajili ya kujigundua binafsi kwa njia ya unajimu.

# Namna 10 za Kufanya Uinjilisti kati ya Washiriki wa Makanisa ya Uongo

1 **Fahamu mafundisho ya msingi ya Biblia.** Hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kujua kila fundisho la uongo la kila kanisa la uongo, lakini Wakristo wajuao Biblia vizuri wanaweza kukuza uwezo wao wa kutambua mafundisho yasiyo sahihi. *Ujue kile unachokiamini na kwa nini unakiamini hivyo.*

2 **Usitegemee kwamba kila mshiriki wa kanisa la uongo anaamini sawa.** Wafuasi wa kundi moja wanaweza kutofautiana kwa kiasi cha kuelewa kwao (au kwa maoni yao). Muulize mtu huyo kuhusu imani yake binafsi; usimshtaki.

3 **Mara nyingi washiriki wa makanisa ya uongo wamefunzwa kujibu.** Kwa mfano, Mashahidi wa Yehova na Wamormoni wanaweza kuonekana kuwa na jibu kwa kila kitu. Lakini, mara nyingi wanachojua tu ni mfumo wa mafundisho ya kanisa lao, marejeo mengine ya Biblia, na hotuba waliyokariri, hotuba ambayo inawafanya waonekane kujua zaidi kuliko wanachojua.

4 **Thibitisha katika Biblia.** Mara nyingi washiriki wa makanisa ya uongo watatumia mistari ya Biblia bila kuzingatia mazingira. Kwa tahadhari, thibitisha maana ya aya wanazotumia kwa kusoma mistari inayotangulia na inayofuata—au bora, usome sura nzima!

5 **Fafanua maana ya maneno.** Makanisa ya uongo mara nyingi hujaribu kubadilisha maana ya maneno ya kawaida ya imani kama "Mungu" na "wokovu." Ili muweze kuelewana vizuri, unaweza ukaanza kwa kufafanua maneno yanayotumika kama vile, "Mungu" maana yake nini, au "wokovu" maana yake nini, n.k.

6 **Uliza maswali yenye kusudi.** Huwezi kumlazimisha mtu kuamini mafundisho ya kweli kama amenaswa na kanisa la uongo. Badala yake, uliza maswali kwa upole ambayo yanaweza kumsababisha kufikiria zaidi kuhusu imani yake.

7 **Uwe na upendo.** Si unachosema tu, bali ni jinsi unavyokisema! Uwe mpole na mwenye heshima kwa wakati wote, hata kama wao wasipokuwa hivyo (Wengine wanadhani watapuuzwa, kubezwa, kufokewa na kudharauliwa).

8 **Thibitisha umungu wa Yesu.** Washiriki wa makanisa ya uongo hushindwa kumtambua Yesu kama anavyostahili, wakikana au kupindua mafundisho ya yeye ni nani na kazi yake ni nini. Fahamu Maandiko yanayoonyesha kwamba Yesu ni Mungu.

9 **Sisitiza injili.** Washiriki wa makanisa ya uongo wanahitaji kusikia ukweli kuhusu neema ya Mungu zaidi kuliko chochote kingine!

10 **Toa ushuhuda wako.** Mungu anaweza kutumia ushuhuda wako kuhusu kile Yesu Kristo alichofanya katika maisha yako ili kubadilisha mawazo na mioyo ya watu.

Haya yameandaliwa kutokana na *10 Keys to Witnessing to Cults* na Ron Rhodes (Rose Publishing, 2008)



Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

# Kwa Nini na Kwa Namna Gani Makanisa ya Uongo Huwatega Watu (hata Wakristo)?

## Nguvu Mbili Zinazoandamana

1. Kuna *mitindo* mbalimbali kanisa la uongo linayotumia kuwanasa watu, kuwazoesha mafundisho yao na kuwashikilia.

2. Kuna udhaifu wa kibinafsi wa mlengwa.
   a. Makanisa ya uongo yanaweza kuvuta watu wa aina zote, hata watu wenye akili nyingi na sura nzuri. Lakini mara nyingi, wale waliopatwa na taabu kubwa na huzuni nyingi (kama vile kuachwa na mwenzi au kifo cha ndugu wa karibu) wako hatarini zaidi kunaswa na kanisa la uongo. (Kundi hilo linaweza kutumia ujanja wa kutambua shida ya mtu mdhaifu na kumbembeleza.)
   b. Watu wanaonaswa na makanisa ya uongo wana uwezo mdogo wa kutambua hatari ya kiroho: “Njia unayodhani kuwa ni sawa, mwishoni yaweza kukuongoza kwenye kifo” (Methali 14:12).
   c. Watu wanaonaswa na makanisa ya uongo wana mahitaji na hamu ambavyo havijatoshelezwa: “kwa mwenye njaa kila kichungu ni kitamu” (Methali 27:7b).

## Kwa Nini Watu Wanajiunga na Makanisa ya Uongo?

1. Sababu za Kielimu
   Watu wana hamu kubwa ya kupata majibu ya maana kwa maswali ya msingi ya maisha yao na kuhusu Biblia. Wanaweza kudanganywa na “utaalamu” wa kibiblia usio wa kweli (k.m. Mashahidi wa Yehova).

2. Sababu za Kihisia
   Watu wanahitaji kupendwa kindugu na kutoyumbayumba kihisia. Wengine wanaweza kushawishika kutafuta upendo ule unaokosekana kwa kushirikiana na kanisa la uongo.

3. Sababu za Kijamii
   Watu wanataka maisha yao yawe na maana na kujiona kuwa sehemu ya kundi ambalo linafanya kitu cha maana.

4. Sababu za Kiroho
   
   Watu mara nyingi wana hamu ya kuwa karibu na Mungu na kuona mambo ya kiroho na miujiza. Wanataka kulipata kanisa lisilo na kifani, ambalo “ni kanisa kikwelikweli.”

## Hatua za Kunaswa na Kanisa la Uongo

1. Udanganyifu (kabla hujajiunga)
   Kanisa la uongo hutoa ahadi nyingi za uongo na huficha mambo yake mabaya.

2. Utegemezi (wakati umejiunga tayari)
   Kanisa la uongo laweza kuanza pole pole kukusababisha usiwaamini ndugu zako, rafiki zako, na wengine na kujitenga nao, hasa wale ambao wangekuonya au wangeogopa kuona wewe unakuwa mfuasi wa kanisa hilo.

3. Huzuni (baada ya muda)
   Kanisa la uongo lakufanya uwe na hofu ya kuharibikiwa kabisa kijamii na kuangamizwa kiroho ukijaribu kutoka kwenye kanisa hilo. Katika makanisa mengine, hakuna njia ya kutoka yenye heshima, na ungeweza kupoteza karibu vyote (pamoja na familia yako, rafiki zako, kazi yako na mali zako) ukipinga matakwa ya kanisa na kutoka.

Haya yameandaliwa kutokana na studies na Michael Langone (International Cultic Studies Association) na Harold Bussél (mchungaji kiinjili)

# Hatari za Kushirikiana na Makanisa ya Uongo

Kuna vuguvugu nyingi za kidini za uongo ambazo zimezuka Afrika ya Mashariki na duniani kote zikidai kwamba zinasambaza ukweli wa Mungu, lakini kweli zinaweza kuwa chimbuko la kuwa na umaskini sugu, familia kutawanyika, kuwa mwehu, kuacha masomo, kuwa na ugonjwa au kuonyesha mwenendo wa ajabu katika maisha yako.

Leo, kama ningeenda katika chuo kikuu na kumwomba mwanafunzi mkristo kuacha masomo yake na kukaa tu nyumbani asubiri ufunuo fulani wa kimungu, kuna wachache sana ambao wangekubali. Kama ningekuja kwako nyumbani ukiwa mke uliyeolewa na kukuambia umwache mume wako kwa sababu yeye si mapenzi ya Mungu kwako, inawezekana ungepiga yowe au kumwita mchungaji wako na kumwambia kwamba nimejaribu kukushawishi kuvunja ahadi yako uliyotoa mbele za Mungu. Nikikuambia kufunga biashara yako na kunipa mimi pesa zako zote, inawezekana ungepigana nami. Na kama ningekuomba kunywa mkojo wangu au sumu, bila shaka ungenishtaki kisheria.

Lakini, baada ya mwaka mmoja au miaka miwili, watu wengi—wasomi na wasio wasomi, matajiri na maskini, viongozi na watu wa kawaida—watashawishika kufanya mambo haya na hata zaidi. Ninamfahamu mwanafunzi mmoja wa Chuo Kikuu cha Nairobi ambaye aliacha masomo yake ya Usanifu wa Majengo (Architecture) mara kabla ya mitihani ya mwisho akiamini kwamba Mungu alikuwa anamwagiza kukaa na kungojea matakwa ya Mungu nyumbani. Ninamfahamu mwanamume ambaye aliwahi kufanya kazi Shirika la Posta aliyeacha kazi akitaja wazo la kwamba ulimwengu umefika mwisho wake na hakuna haja ya kuendelea kufanya kazi. Ninawafahamu wanawake kadhaa ambao waliwahi kuhudhuria mikutano ya aliyejiita “nabii” na walihimizwa kila wakati kuwaacha waume zao na kutoa pete zao za kufunga ndoa kwa sababu waume wale hawakuwa mapenzi ya Mungu kwao. Viongozi wengine wa Mashahidi wa Yehova




wamewahi kuwahimiza wake au waume kuwapa wenzi wao talaka kama wenzi hao wasingetaka kuwa Mashahidi.  Mfano mwingine ni moto wa Kanungu, tukio la kusikitisha la kuchomwa moto watu huko Kanungu, Uganda, moto uliosababisha vifo vya karibu watu elfu moja (1,000). Kibwetere,



ACFAR
Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.
Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

aliye kiongozi wa "The Movement for the Restoration of the Ten Commandments of God" ("Vuguvugu ya Kurudisha Amri Kumi za Mungu"), aliwaagiza washiriki wake kuuza mali zao, kufunga biashara zao na kumpa pesa zao, kwa sababu dunia ilikuwa imefika kikomo chake katika mileniumu (katika mwaka 2000).

Basi, kitu gani kinamsababisha mtu aliyekataa kufanya yale yaliyotajwa juu ayafanye na kuwahimiza wengine wajiunge naye muda wa mwaka mmoja au miaka miwili ukipita? Ni kitu kimoja kidogo: kauli zihusuzo Mungu. Mara linapotajwa jina la Mungu, ni kama macho na masikio yetu yanazibwa, na hamu ya kujua zaidi inaibuka. Inavutia zaidi kama kauli hizo zimejaa ahadi za mafanikio ya kimwili au kijamii. Mara zingine, ni ahadi ya kuwa na mamlaka ya kiroho, mtu akipanda ngazi ya kiroho ya kufahamika kuwa mkubwa zaidi kuliko wale wengine wadogo ambao ni sehemu ya kundi lilelile. Biblia ikitajwa tu, wengi watapumzisha akili zao na hawatakosoa kinachosemwa. Kwa hiyo, mwanafunzi au mwalimu anaweza kuwa na akili nyingi, lakini matumizi ya maneno ya kiroho na ahadi vinamfanya kuwa punguani. Hapo tunaweza kuona umuhimu wa kusoma Biblia mara kwa mara ili



matapeli na wanaojidai kuwa walimu wa kiroho wasitumie aya za Biblia tofauti na maana yake kuwatega watu waaminifu wa Mungu.

## Hatari Zingine za Kujiunga na Kanisa la Uongo:

**1. Makanisa ya Uongo yanaweza kusababisha kifo chako.** Mara nyingi kupitia mahubiri yanayosisitiza ujio wa Kristo kuwa karibu, na hasa kuhusu mwisho wa dunia kuwa karibu, makundi kama haya yamewahi kuwadanganya watu wanywe sumu, kama tukio mwaka 1978 katika mji wa Jonestown, Guyana, wakati Jim Jones aliwaongoza watu 913 wanywe sumu. Katika Moto wa Kanungu wafuasi karibu elfu moja (1,000) wa Joseph Kibwetere walikufa. Kama kundi "Nyumba ya Yahweh" lisingesimamishwa katika Kenya, wengi wangekufa. Makanisa mengine ya uongo yatawatenga watu bila chakula au kuwahimiza wafunge bila kikomo mpaka wamefika hali ya utapiamlo au mpaka kufa. Katika ulimwengu ambao magaidi wanajilipua wakiamini wanamfanyia Mungu jema—watu walio wasomi na wasio wasomi—hatuwezi kuacha kusisitiza kipengele hiki tusije tukafa huku tunajiona.

**2. Makanisa ya Uongo yanaweza kuvunja nyumba yako kesho.** Katika miaka 1990, nilimfahamu mwanaume fulani huko Thika ambaye mke wake alihudhuria kanisa la uongo. Aliyakubali mafundisho ya kanisa hilo kiasi cha kwamba aliwaona familia yake kama maadui dhidi ya mpango wa Mungu kwa ajili yake. Aliondoka nyumbani

wakati mtoto wake wa kike alipokuwa na miezi miwili. Mama alipotambua kosa lake, mtoto wake alikuwa na karibu miaka kumi. Marafiki, ndugu, askari wa polisi na wengine wema walijaribu kumrudisha nyumbani bila mafanikio. Nilikuwa ninahutubia kule Teso miaka kadhaa iliyopita niliposikia kuhusu kundi ambalo lilikuwa linavunja nyumba katika jina la Mungu. Mara zingine, wanawake



walihimizwa wawaache waume wao na kuwa wake za kiongozi wa kanisa la uongo.

**3. Makanisa ya Uongo yanaweza kukufanya kuwa maskini mara moja.** Ujumbe unaoitwa "Injili ya Mafanikio" umetapakaa katika maduka mengi ya vitabu. Wanaume na wanawake wenye tamaa ya fedha wanaojisingizia kuwa watumishi wa Kristo wanachukua mali zote za watu na kufanya mapato ya watu yawe kama watumwa wao, vyote vikitendeka kama ni kumtolea Mungu. Maandiko kama Malaki 2:16 na Luka 6:38–39 yanatumiwa vibaya ili kuwaibia maelfu ya watu pesa na mali zao walizopata kwa nguvu nyingi. Kauli kama "Toa mpaka usikie uchungu," na "Usimpe Mungu ambacho hakijakugharimu," na "Mjaribu Mungu uone kama hatakubariki," na "Mbariki mtumishi wa Mungu," zinatumika kulaghai waaminifu wa Mungu. Shida ni kwamba, wakati wengi wanatoa nauli zao za basi, mishahara na mali, ni yule tu anayetolewa ndiye anayefanikiwa, si wale wanaotoa. Njia rahisi sana kuliko zote ya kuendelea kuwadanganya waumini ni kutumia vibaya Maandiko katika Marko 10:29 wanapoambiwa wakitoa watapewa mara sitini na mara mia. Tena, mara nyingi, waumini wengi wanashawishika mno kwa kufikiria kupokea, ndio maana wanadanganyika kirahisi kutoa mali zao. Tunapaswa kuchukua tahadhari sana kuhusu uongo mwingi unaoahidi mapato ya haraka. Msemo wa kiingereza unafaa hapa: "If a deal is too good, think twice" (yaani, "Kama fursa ni nzuri sana, fikiria mara mbili."). Chukua tahadhari kuhusu kutoa pesa kwa ajili ya maombi. Jihadhari kuhusu "kupanda mbegu za pesa" na ujanja wa hivi karibuni kuhusu kununua mafuta ya upako. Hii ni michezo ya kiuchumi, na si kuwekeza kiroho.

**4. Makanisa ya kiroho yanaweza kusababisha magonjwa ya kimwili na ya kiakili.** Wengi waishio katika himaya ya kanisa la uongo wana lishe



AC|FAR
Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.
Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

mbaya isababishayo utapiamlo. Wengine walioishi kwenye himaya ya kanisa la uongo wamewahi kupata maradhi ya kuona vitu visivyokuwepo au kuwa wehu. Mara zingine, hasa katika kanda ya Nyanza huko Kenya, wengine waaminifu walianza kukaa na viogozi wa kanisa la uongo, wakapata ukimwi. Katika Uganda na mara zingine Kenya, nguvu za dola zimewahi kuingia na kuwaokoa watu kutoka makambi kama haya. Mazoea ya makanisa ya uongo yamewahi kusababisha washiriki wake kubweka kama mbwa au kunguruma kama simba wakidai kwamba wamepata uelewa wa kiroho wa ndani zaidi au wanaabudu kwa dhati. Maradhi ya kawaida zaidi kwa mshiriki wa kanisa la uongo ni kuvunjika moyo, hali ambayo inaweza kusababisha kifo.

## Mapendekezo ya Kujikinga Dhidi ya Makanisa ya Uongo:

Kwanza, **wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao Neno la Mungu na kuanza wakiwa wadogo**. Kusoma Neno la Mungu pamoja baada au kabla ya chakula cha jioni kuna nguvu. Wakati watoto wanapojua neno kwa kina,



ni vigumu sana kwao kudanganywa. Wazazi wenyewe watapata faida ya kiroho katika ukweli wa Mungu pia.

Pili, **kila mtu anapaswa kuwa na Biblia na kuisoma.** Wale ambao wazazi wao au ndugu hawajui kusoma wanapaswa kuwasomea, au kuwapatia mikanda ya kusikiliza Biblia au Biblia iliyo na picha.



Tatu, **lazima tujizoeshe kuwa na akili ya kuyakosoa mafundisho na kuuliza maswali kabla ya kuyakubali au kuyaamini**. Ni ile hali ya kuwa mwepesi wa kuamini chochote ambayo inatumiwa sana na makanisa ya uongo kuwanasa watu.

Mwishowe, **tuepukane na hamu ya mafanikio ya moja kwa moja na njia za mafanikio ambazo hazitegemei juhudi au bidii.** Tunapaswa kukumbuka kwamba Mungu si ATM (mashine inayotoa pesa kwenye benki). Lazima tujifunze kumwabudu, tukijua kwamba yeye ni Mungu wa ukweli. Zaidi ya hayo, lazima tuyakimbie makundi yanayowashawishi watu kwa kutumia mitindo ya shoo na ya burudani. ***Tukipenda Neno la Mungu, tutatambua kirahisi lile bandia.***

Haya yameandaliwa kutokana na “The Dangers of Cultic Involvement” na Reuben Kigame (Word of Truth Ministries).

# Jinsi Watu Wanavyokwepa Wajibu wa Kupima Mafundisho

Kazi ya kupima mafundisho kuhusu Mungu na Biblia imepuuzwa na kudharauliwa sana na watu wanaojiita Wakristo siku hizi. Kuna watu wengine walio wakosoaji sana wa mtu yeyote anayepima mafundisho kuhusu Mungu kwa kutumia Neno lake, na hawataki mafundisho yao yapimwe na ukweli wa Biblia. Sababu ni rahisi mara nyingi: mafundisho yao hayawezi kusimama yakipimwa na misingi ya kibiblia.

Labda tungetarajia kwamba makundi ya kidini ambayo ni ya uongo kabisa na ambayo yanajidai kuwa Wakristo wa kweli wa pekee yangejaribu kuwazuia watu wasipate uwezo wa kutambua mafundisho yaliyo ya kweli na yaliyo ya uongo. Lakini kinachosikitisha ni kugundua kwamba watu wengi katika makanisa ya kiinjili pia wanapuuza zoezi la kujizoesha kutambua ya kweli na ya uongo. Hapo chini kuna hoja zingine ambazo zinatumika sana kukwepa wajibu wa kupima mafundisho.

## "Usisababishe Mafarakano katika Mwili wa Kristo"

Wakati mafundisho ya mwalimu au kiongozi anayejiita kuwa Mkristo yanapimwa au yanakosolewa, hakika utasikia mtu akilalamika kwamba ukosoaji huo unasababisha mafarakano katika Mwili wa Kristo. Mkosoaji atashtakiwa ikisemekana kwamba "anapanda mbegu za fitina kati ya ndugu" (msemo kutoka Methali 6:19), na anasababisha mafarakano na matengano. Mara zingine, wamesema kweli juu yake.

Ni kweli mara zingine watu wanaokosoa mafundisho ya wengine wanasababisha fitina tu. Mara zingine watu wanasababisha fujo na hali ya kuchanganyikiwa kwa kusisitiza kupita kiasi tofauti zilizopo za kiimani. Kusababisha fitina ni dhambi, dhambi ambayo watu wanaojaribu kupima mafundisho kuhusu Mungu lazima waepukane nayo kwa dhati. Lakini, matengano yote si dhambi. Wakristo wanapaswa kujitenga kidini na wapotevu. Kanisa lina *jukumu* (na si haki tu) la kujitenga na kundi la watu likiibuka na kuanza kusambaza mafundisho ya uongo, mafundisho wanayoyafuata hawawezi kuhesabiwa kuwa Wakristo tena.

Hata kama wale wanaoyaamini mafundisho hayo ya uongo ni Wakristo, kama kosa ni baya la kutosha, kanisa lazima lisimame kwa upande wa ukweli unaotengana





Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

na mafundisho ya uongo na wale wanaosisitiza kuyafundisha.

Katika Waroma 16:17, Paulo aliandika, “Ndugu zangu, nawasihi mwafichue wote wanaosababisha mafarakano na kuwafanya watu wengine waanguke, *kinyume cha mafundisho mliyofundishwa*. Jiepushe na watu hao.” Ni nani, kwa mujibu wa Paulo, anayesababisha mafarakano? Je, ni wale wanaofundisha mafundisho ya uongo na yaliyo tofauti, au ni wale wanaofichua mafundisho ya uongo? Ni wazi kabisa kwamba ni wale wanaofundisha mafundisho ya uongo. Wale wanaopiga yowe dhidi ya walimu wa uongo katika kanisa *si* wasababisha mafarakano.

Au, tupate mtazamo mwingine. Tuwaze kwamba katika kanisa fulani kuna makundi mawili. Kundi la kwanza linakubali mafundisho yaleyale ambayo kanisa lilikuwa limefundisha tangu lilipoasisiwa. Kundi la pili linafuata mafundisho mengine yaliyoingizwa na mwalimu mpya. Mafungo haya mawili ya mafundisho yanatofautiana sana—kiasi cha kwamba ni mawazo mawili tofauti yanayopingana kabisa kuhusu maana ya kuwa Mkristo. Katika hali hiyo, tumekuwa na nini? Tayari kuna utengano katika kanisa. Haiwezekani kuepukana nao. Makundi haya mawili hayawezi kuwa na umoja. Kama mafundisho yao yanatofautiana kiasi cha kutosha, watakuwa na mawazo mawili tofauti kuhusu maombi, hata hawawezi kuomba pamoja.

Katika kesi kama hiyo, hakuna shida katika kubainisha na kutambua kilicho kweli. Si kusababisha mafarakano ukitambua kwamba tayari kuna mafarakano. Aidha hakuna shida kwa kundi moja kudai kwamba mafundisho yao ni ya kweli na yale ya kundi jingine ni ya uongo. Makundi yote mawili hayawezi kuwa sahihi.

Tunapaswa kuhakikisha hatujitengi kuhusu mambo madogomadogo. Lakini pia, hatuwezi kuwa na umoja kama tumepuuza ukweli. “Umoja wa imani” lazima utunzwe kwa ujuzi mzuri wa mafundisho ya kikristo (Waefeso 4:15–16). Mara nyingi wale walimu wanaolalamikia umoja kuvunjika kwa mwili wa Kristo wameuvunja kwa kufundisha mafundisho ya uongo.

## “Usimguse Mpakwa Mafuta wa Mungu”

Wakati Wakristo wakianza kutaja wasiwasi wao kuhusu mafundisho yanayosambazwa na wahubiri wanaojiita Wakristo, utasikia mara nyingi, “Usimguse mpakwa mafuta wa Mungu!” Mara mbili katika Biblia twasoma kwamba Mungu anasema, “Msiwaguse wapakwa mafuta wangu; msiwadhuru manabii wangu” (1 Nyakati 16:22; Zaburi 105:15). Msemo huu ukitumiwa na walimu wengine siku hizi, wanamaanisha kwamba hakuna mtu yeyote ila Mungu aliye na haki ya kuhukumu au kukosoa hadharani mafundisho ya walimu fulani maalumu, wanaotambulika kuwa “wapakwa mafuta” wa Mungu.

Tuseme nini kuhusu wazo hili? Mahali pa kuanzia ni aya hizi za Biblia zenyewe. Ukisoma aya hizi kulingana na mazingira

yake, “wapakwa mafuta” ni mababu wa Israeli—Abrahamu, Isaka, na Yakobo (1 Nyakati 16:15–21; Zaburi 105:6–14). Haijaeleweka kwa nini wanaitwa “wapakwa mafuta” wa Mungu. Inaonekana kwamba neno “wapakwa mafuta” lina maana sawa na neno “manabii” linalotumika katika mstari uleule. Ingawa matumizi ya neno hili hivyo ni machache, kuna sehemu zingine pia ambazo zinagundulika (1 Wafalme 19:16b; Isaya 61:1). Pia, maana hiyo inaandamana na mazingira ya aya, kwa kuwa msisitizo wa aya ni kazi ya pekee mababu wa Israeli waliyofanya kuwa wale waliopewa neno la Mungu, yaani agano, likaundwa taifa la Israeli.

Kwa upande mwingine, ni wazi kwamba mababu wa Israeli walikuwa *zaidi* ya manabii. Walikuwa wanaume walioahidiwa kwamba wazawa wao wangekuwa pamoja na wafalme ambao wangetawala nchi ya Kanaani (Zaburi 105:11; Mwanzo 17:6, 16; 35:11). Wazo hili pia linaambatana na ukweli wa kwamba wakati Agano la Kale linapoongelea “wapakwa mafuta” wa Mungu, karibu kila wakati linarejea wafalme (k.m. 1 Samueli 2:10, 35; 2 Samueli 1:14, 16; Zaburi 2:2; 89:38, 51; Danieli 9:25, 26; tz. 1 Samueli 16:12, 15; 1 Nyakati 11:3; 14:8; 29:22; Isaya 45:1).

Ni wazi kwamba “wapakwa mafuta” ambao Mungu amesema “wasiguswe” *si* walimu, wahubiri, wainjilisti, au viongozi wa kidini tu. Walikuwa watu wa pekee katika historia ya Israeli waliopewa mamlaka ya kinabii na kifalme na hadhi ya juu.

Kweli, kuna walimu wengine ambao wanajidai pia kuwa manabii—wasemaji maalumu ambao kupitia kwao Mungu ananena siku hizi. Lakini, watu wanajaribu kunukuu mstari huu wa “Msiguse wapakwa mafuta wangu” na kuutumia kwa ajili *ya mtu yeyote* wanayemwamini kuwa mwalimu au mtumishi mwenye vipaji vya kiroho. Matumizi ya namna hii yanapinga wazi maana ya aya.

Wazo jingine linahitaji kutajwa hapa. Kilichopigwa marufuku na Mungu katika mstari huu ni wafalme wapagani kuwaua au kuwadhuru “wapakwa mafuta” wa Mungu. Mungu hakupiga marufuku kuweka wazi makosa ya wapakwa mafuta hawa. Kwa mfano, katika Mwanzo 20:7 Mungu alimwonya Abimeleki, mfalme wa Gerari, kumrudisha Sara kwa Abrahamu, kwa kuwa “Abrahamu ni nabii.” Lakini hili halikumzuia Abimeleki amkemee Abrahamu kwa udanganyifu wake (m. 9–10). Ni kitu kimoja kumdhuru mpakwa mafuta wa Mungu; ni kingine kubainisha makosa yake. Hata manabii wasipokuwa wanaongea kinabii wanaweza kukosea (k.m. 2 Samueli 7:3, tz. 4–17).

Ni kweli tunapaswa kutowakataa manabii wa Mungu, bado tumebaki na jukumu la



Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.
ACFAR
Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

kutambua manabii wake wa kweli ni akina nani. Si kila mmoja anayejidai kuwa nabii wa Mungu siku hizi ni nabii wa kweli, kwa kuwa mara nyingi wanapingana wao kwa wao. Mtu akijidai kuwa nabii wa Mungu lakini anafundisha mafundisho ya uongo au anatangaza unabii wa uongo, tuna kila sababu ya kumkataa—kweli, ni lazima tumkatae (Kumbukumbu 13:1–5; 18:20–22).

Katika Agano Jipya, "Mpakwa Mafuta" ni Yesu Kristo, aliye nabii, kuhani, na mfalme na mfano. Wale waliounganа na Kristo kupitia Roho wake kwa namna fulani ni "wapakwa mafuta" (2 Wakorintho 1:21). Kwa sababu hiyo, hatuhitaji walimu "wapakwa" walio na ufunuo wa siri na wenye kujidai kuwa na mamlaka maalumu wakituambia tuwaamini (1 Yohane 2:20, 27).

Mwisho wa yote ni huu: Agano Jipya linatuambia wazi kuwakemea walimu wa uongo katika kanisa (Waroma 16:17; 1 Timotheo 1:3; Tito 1:11; 3:10–11). Kwa hiyo, hakuna mtu yeyote aliye na haki ya kutopimwa na kwa sababu ni "mpakwa mafuta wa Mungu." Kama mtu anafundisha mafundisho ya uongo, hakika yeye si mpakwa mafuta wa Mungu kwa namna yoyote ile.

## "Angalia Matunda!"

Mtu kuwa mwalimu wa kweli au wa uongo kunatambulika kulingana na mafundisho yake. Ingawa ukweli huu uko wazi, watu wengine wanakataa. Wengine wanaojiita Wakristo siku hizi wana hoja ya kwamba walimu na watumishi wapimwe kulingana na "matunda" ya huduma zao, na si kwa kulinganisha na kutofautisha mafundisho yao na mafundisho ya Biblia.

Kwanza—wazo hili lifahamike—kudai kwamba mafundisho yapimwe kulingana na "matunda," au matokeo yake, ni fundisho linalohitaji kupimwa. Lazima tutambue kama fundisho hili ni kweli kabla hatujaanza kulitumia kupima mafundisho mengine na watu wanaoyafundisha.

Mstari unaotumiwa kama msingi wa kauli hii unafahamika sana. Yesu mwenyewe alisema tungetambua manabii wa uongo "kulingana na matunda yao…Mti mzuri hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mbaya hauwezi kuzaa matunda mazuri. Kwa hiyo, mtawatambua kwa matunda yao" (Mathayo 7:15–20).

Kama hoja mbili zingine zilizotajwa tayari dhidi ya kupima mafundisho, hata hii ina msingi katika Biblia. Ni dhahiri kwamba kama Yesu mwenyewe alisema tunaweza kutambua manabii wa uongo kwa matunda yao, ni kipimo sahihi.

Shida ni kwamba watu wengine wanatumia aya hii kama njia ya kuepukana na kupimwa kwa mafundisho yao. Kumbuka kwamba kuna aya zingine katika Biblia zinazowaagiza Wakristo kuwapima *kimafundisho* walimu wanaojiita Wakristo (k.m. 1 Yohane 4:1–2). Yesu hamaanishi kwamba mafundisho yenyewe hayawezi kutumiwa ili kupima kauli ya mtu kujidai kuwa nabii. Badala yake, ni bora tumwelewe kumaanisha kwamba kupima

matunda ya huduma ya mtu ni njia *moja* (kati ya njia kadhaa) kutambua ukweli wa kauli ya mtu.

Tunda moja baya la mafundisho ya uongo ni kwamba yanasababisha mafarakano. Tena, si hatia ya wale wanaokosoa mafundisho ya uongo—ni hatia ya wale wanaoyafundisha. Itakuwa jambo la ajabu kuanza kuwalaumu wale wanaokosoa mafundisho ya uongo kana kwamba wao ndio wanaosababisha mafarakano!

Hata madai ya kuwa na "matunda mazuri" yanayotolewa na makundi mengine yanayofuata mafundisho ya uongo lazima yapimwe. Kwa mfano, makundi mengi ya kidini yanadai kwamba wafuasi wao wamepata kuwa na upendo zaidi, furaha zaidi na kujiamini zaidi. Shida hapa ni kwamba ni vigumu kuthibitisha madai hayo. Watu wanaweza waonyeshe machoni pa watu wengine hisia za uchangamfu, upendo, furaha, na kujiamini, lakini ndani yao hawako hivyo kabisa. Tafadhali uelewe kwamba sikatai Ukristo wa kweli ni bora kabisa kwa sababu hiyo. Hoja yangu ni kwamba upendo, furaha, na kujiamini vinaweza kuwapata wasio Wakristo kwa kiwango cha kawaida, na hili lisitambuliwe kuwa sawa na faida za kumfahamu Yesu Kristo wa kweli.

Vilevile, makundi mengine yanayoamini mafundisho ya uongo yanadai kwamba imani yao lazima iwe ya kweli kwa kuwa wamekuwa na miujiza miongoni mwao—hasa kuponywa kwa watu. Lakini, Biblia iko wazi ikituonya kwamba viongozi wa kidini wa uongo wataweza mara zingine kufanya ishara za uongo na maajabu (Mathayo 24:24; 2 Wathesalonike 2:9). Agano la Kale huonya kwamba Mungu mara zingine alimruhusu nabii wa uongo kufanya ishara au maajabu ili kuona kama watu walikuwa na hamu zaidi kuona miujiza iliyoshangaza kuliko kumjua Mungu wa kweli (Kumbukumbu 15:1–5). Kwa hiyo, hatupaswi kuamini miujiza ni uthibitisho wa moja kwa moja kwamba mafundisho ya mtu yametoka kwa Mungu.

Nikisema kwamba walimu wa uongo wanaweza kufanya yanayoonekana kuwa miujiza,.... simaanishi kwamba kila habari ya miujiza inayohusiana na mafundisho ya uongo lazima "miujiza" ile itokane na Ibilisi. Hatutaweza kila wakati kujua kama ni miujiza ya kweli—ambayo itambuliwe kuwa ya kishetani—au la. Miujiza ya uongo inaweza kufanywa na matapeli, au labda ni uponyaji unaosababishwa na mabadiliko ya mtazamo wa mtu (sababu za kisaikolojia). Au labda kuna uwezekano wa kwamba Mungu angemponya mtu aliyesikiliza mafundisho ya uongo lakini hakuelewa maana yake na ambaye alimwamini Mungu wa kweli na nguvu zake. Si muhimu sana kuwa kujua kila wakati sababu ni nini. Kilicho muhimu ni kwamba kutokea kwa yanayoonekana kuwa miujiza si kibali cha



Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.

AC/FAR

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

# Jinsi Watu Wanavyochenga Wajibu wa Kupima Mafundisho

Mungu kwa kila alichofundisha kiongozi wa kidini anayehusika

## "Usitaje Majina!"

Mara zingine viogozi wa kikristo wako tayari kuruhusu ukosoaji wa mafundisho fulani yasipotajwa majina ya walimu walioyafundisha. Wazo ni kwamba kukataa fundisho fulani si kusababisha mafarakano, lakini kutaja jina la mtu kama mwalimu wa uongo ni kusababisha mafarakano.

Hoja hii inamaanisha kwamba si sahihi kusababisha "utengano" katika kanisa unaohusu mambo ya kimafundisho. Kama fundisho fulani ni baya kiasi cha kufanya kanisa lilikatae, hii inamaanisha hata wale



pia wanaosisitiza kuendelea kulifundisha watambuliwe na kufichuliwa.

Mfano wa Paulo unasaidia. Mara zingine aliamua kutotaja majina ya walimu wa uongo (k.m. 1 Timotheo 1:3). Lakini nyakati zingine anatoa majina yao. Kwa mfano, katika barua moja, alitaja Himenayo na Aleksanda (1 Timotheo 1:20) na katika barua nyingine alitaja Himenayo tena pamoja na Fileto (2 Timotheo 2:17). Inaonekana kwamba hakuna shida kutaja majina ya walimu wa uongo.

Sababu moja ya umuhimu wa kutaja majina ya walimu wa uongo ni kwamba kama mafundisho ya uongo yanazungumziwa kwa juujuu, mara nyingi watu watakataa kwamba walimu wao wanayasambaza. Hawataamini kwamba walimu wao wapendwa wanafundisha mafundisho ya uongo mpaka maneno yao yanukuliwe kutoka kwenye maandishi yao na mahubiri yao.

Kama mtu ni mwalimu wa uongo asiyetubu, tunahitaji kufanya zaidi ya kukataa mafundisho yake tu. Tunahitaji kujiepusha na yule mtu kabisa. "Mtu anayesababisha mafarakano mpe onyo la kwanza na la pili, kisha achana naye. Wajua kwamba mtu wa namna hiyo amepotoka kabisa, na dhambi zake zathibitisha kwamba amekosea" (Tito 3:10–11). Maneno haya ni magumu, na ni makali, lakini ni maneno ya Mungu. Mtu anayesababisha mafarakano kwa kufundisha mafundisho yaliyo tofauti na ya uongo akataliwe. Ili kanisa liwe na msimamo mmoja, mwalimu wa uongo atajwe hadharani.

Haya yameandaliwa kutokana na *Orthodoxy and Heresy: A Biblical Guide to Doctrinal Discernment* na Robert M. Bowman, Jr. (Baker, 1992)

# Je, Tuwategemee Malaika kwa Msaada wa Kiroho?

**Watu Wanasema:**

Watu wengine siku hizi wanasema tuwategemee malaika kutusaidia kutueleza kuhusu sisi wanadamu, kuhusu Mungu, kuhusu mbinguni, namna gani tuishi, namna gani tupate uponyaji wa magonjwa, n.k. Kuna vitabu kadhaa vinavyoelezea, mfano Waulize Malaika Wako, Ujumbe toka kwa Malaika Wako, au Majibu toka kwa Malaika. Wale wanowategemea malaika hivyo huwaita "wasaidizi wa kiroho" au hata "bachwezi" (Uganda).

**Lakini Biblia inasema:**

**Si Kawaida ya Malaika Kuongea na Binadamu.**

Katika Biblia hatuoni mtu yeyote aliyewatafuta malaika ili kuwasiliana nao au kutafuta ili wampe ujumbe wake toka kwao. Malaika walipotokea kwa watu ilikuwa ni jambo la mshangao kwao na si kawaida. Maneno ya utangulizi ya malaika anapowatokea watu, mara nyingi, huwa "Usiogope" (k.m. Mwanzo 21:17, Mathayo 28:5; Luka 1:13, 30; 2:10).

Kumbuka, si malaika wote wako upande wa Mungu. Kuna roho nyingi za uovu—mashetani—ambao ni mapepo, yaani malaika walioanguka na Ibilisi (Mathayo 25:41). Huwezi kuamini na usiamini kila unalosikia kutoka kwa malaika kama ambavyo huwezi kuamini kila unalosikia kwa watu. Pia ufahamu kuwa Shetani hawezi kukujia akiwa amevaa kifuani mwake lebo kubwa nyekundu iliyoandikwa kwa maandishi makubwa "SHETANI." Ni mjanja, atajibadilisha afanane na malaika wa nuru (2 Wakorintho 11:14).

Maandiko Matakatifu ndiyo njia anayotumia Mungu kuuleta ujumbe wake wa ukweli kwa watu wake wote, kipimo ambacho tunapaswa kukitumia kupima dini zote (Mathayo 22:29, Matendo 17:11; 2 Timotheo 3:16). Hata malaika wanapoongea na watu, hawaongei kinyume na Biblia. Mtume Paulo anawaonya Wakristo wasiikubali injili nyingine, hata kama inatoka kwa malaika (Wagalatia 1:6–9).

Haya yameandaliwa kutokana na *10 Questions & Answers About Angels* na Robert M. Bowman, Jr. (Rose Publishing, 2008)

## LAZIMA PIA UFAHAMU…

Kutafuta mawasiliano na malaika kunafungua mlango wa hatari ya kuathiriwa vibaya na mapepo. Kwa sababu kwa kawaida Mungu hawatumii malaika wake kama njia ya mawasiliano ya moja kwa moja na watu, ujue kuwa Shetani anaweza akachukua hiyo nafasi. Unaweza ukadhani umepata majibu kutoka kwa Mungu kupitia malaika kumbe umesikia sauti za uongo toka kwa malaika wa Shetani. Watu wengine watajaribu kutumia roho za udanganyifu wapate kujua taarifa zilizofichwa au kuwa na nguvu zisizo za kawaida, hasa kwa kupitia mawasiliano na mapepo. Mungu anakataa mambo haya (Kumbukumbu 18:10–12).

AC|FAR

Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

# Je, Tutarajie kwamba Malaika Watatutembelea?

**Watu wanasema...**

Malaika hujitokeza kila wakati. Mwandishi mmoja amewahi kusema, “Wale wanaotaka na walio tayari kuwaona malaika watawaona.”

Waebrania 13:2 husema, “Msisahau kuwakaribisha wageni; maana kwa kufanya hivyo watu wengine walipata kuwakaribisha malaika bila kujua.” Watu wengine wanaamini maana yake ni kwamba sisi *sote* tumewahi kuwaona malaika—bila kujua.”

**Lakini Biblia husema...**

**Kuonekana kwa malaika ni muhimu na ni mara chache.** Ingawa Biblia inaeleza historia ya malaika kujitokeza kwa binadamu, tukichunguza aya hizi tutaona kwamba matukio ya namna hii—hata katika nyakati za Biblia—yalikuwa machache sana, na tunasadiki yangekuwa mara chache siku hizi pia.

Malaika walijitokeza kutangaza kuzaliwa kwa ajabu kwa watu muhimu (Isaka, Yohane Mbatizaji, na Yesu mwenyewe), kuwaita manabii na viongozi wengine kufanya huduma (Isaya), kuleta ufunuo (Ezekieli, Yohane), kuwaokoa au kuwaimarisha manabii (Elia, Elisha, Danieli) na mitume (Petro, Paulo), kutangaza ufufuo wa Yesu kwa wanawake kaburini, na nyakati zingine zenye maana. Karibu wote hawa waliweza kuona malaika mara moja katika maisha yao yote. Biblia haifundishi au kudokeza kwamba tunapaswa kutarajia malaika kututembelea au kujitokeza kwa sababu za kawaida.

Hoja kuu ya Waebrania 13:2 ni kwamba tunapaswa kuonyesha ukarimu kwa wageni, na si kwamba tutakutana na malaika kwa kawaida. Inawezekana kwamba mstari huu unarejea ukarimu alioonyesha Loti kwa wageni ambao walionekana badaye kuwa malaika (Mwanzo 19). Kweli, mtu hajui mgeni atakuwa nani, lakini wageni kuwa malaika si kawaida.

Zaidi ya hayo yote, Wakristo wanapaswa kuepukana na mivuto ya kukazia kwa matumaini yao na nguvu zao uwezekano wa kukutana na malaika, wakati wana uhusiano wa kibinafsi na Mungu ulio wa karibu, aliye *Muumba* wa malaika (1 Petro 1:8–12).

Haya yameandaliwa kutokana na *10 Questions & Answers About Angels* na Robert M. Bowman, Jr. (Rose Publishing, 2008)

## Lazima Pia Ufahamu...

Wazo la kudhani kuwa watu fulani katika huduma ya malaika wana uwezekano mkubwa wa kuwaona malaika halina msingi katika maandiko. Tumeona karibu mara zote ambapo malaika alitokea kwa watu ilikuwa si kwa kutarajia, ni kwa kushitukiza. Hatuoni kwenye Biblia mtu yeyote akiomba akutane na malaika au aonane naye ili amsaidie jambo lolote.

# SWALI: Kwa namna gani tunaweza kutambua nguvu na uwezo wa mapepo?

**JIBU:** Tunaweza kutambua kwa ***maneno***, kwa ***matendo***, na kwa ***muonekano***.

Kwanza, **Shetani anatumia *maneno* yasiyowiana na Maandiko na yanayosambaza maarifa ya uongo**. Ndivyo ilivyokuwa wakati Shetani alipomjia Eva, akapinga kabisa alichoambiwa na Mungu (Mwanzo 3:4). Tena, ilikuwa hivyo wakati Yesu alipomkemea Petro kwa kusema, "Ondoka mbele yangu, Shetani! Wewe ni kikwazo kwangu. Mawazo yako si ya kimungu ila ni ya kibinadamu" (Mathayo 16:23), kwa kuwa Petro alikana kwamba Yesu angekufa. Yesu alitambua kwamba mawazo yaliyokuwa chanzo cha maneno ya Petro yalikuwa ya kishetani. Kila neno kuhusu Mungu au ambalo linadai kwamba limetoka kwa Mungu lipimwe kwa makini katika mwanga wa Biblia.

Pili, **kama vile Yesu alivyoweza kufanya miujiza, ndivyo wanavyoweza Shetani na mapepo wake kufanya miujiza**. Mstari wa 2 Wathesalonike 2:9 unatuonya kwamba, "Huyo Mwovu atakuja na nguvu za miujiza na maajabu ya uongo." Katika siku za mwisho, Yesu huonya, "Watatokea kina Kristo wa uongo na manabii wa uongo. Watafanya ishara kubwa na maajabu ya kuweza kuwapotosha ikiwezekana hata wateule wa Mungu" (Mathayo 24:24). Matendo, hata yakiwa ya ajabu sana au yakionekana kuwa msaada sana, lazima yapimwe na Neno la Mungu.

Tatu, **Shetani na mapepo wake wanaweza kutambulika kwa *muonekano* wake**. Shetani anavamia jumuiya ya kikristo kupitia walimu na viongozi wanaopotosha ukweli. Hakika watu kama hao wataingiza mafundisho yaliyo kinyume cha Maandiko. Katika Matendo 16, Paulo na Sila walimkuta binti mtumwa aliyepagawa na pepo mwenye uwezo wa kuagua. Kwa siku nyingi aliwafuata mitume akilia, "Hawa watu ni watumishi wa Mungu Mkuu. Wanawatangazieni njia ya wokovu" (Matendo 16:17). Ingawa maneno yake yalikuwa kweli, roho aliyeyasababisha alikuwa wa uongo na alitaka kuwanasa watu kwa kiasi kidogo cha ukweli ili nafasi iwepo ya kuilaumu Injili badaye. Paulo alipima maneno yake kuwa ya kweli lakini alijua kwa muonekano wake kwamba mapepo waliomwongoza hawakuwa wa kweli. Hakudanganywa na muonekano uliokuwa ungeweza kuwa wa kimungu. Kwa hiyo, lazima muonekano upimwe kwa makini na Maandiko.

Haya yameandaliwa kutokana na *The Discipline of Spiritual Discernment* na Tim Challies (Crossway, 2007)



Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA

www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

# Tofauti Zilizopo kati ya Makanisa ya Kweli na Makanisa ya Uongo

- Makanisa ya kweli husisitiza mamlaka ya Maandiko (2 Timotheo 3:16–17). *Mara nyingi makanisa ya uongo husisitiza mamlaka ya viongozi wanaodai kwamba wamepokea ufunuo mwingine kutoka kwa Mungu.*
- Makanisa ya kweli husimamiwa na watu wanaoongoza kikweli lakini ni kwa mfano wa upole, kwa mafundisho, na kwa kutia moyo (2 Timotheo 2:24–25; 1 Petro 5:1–3). *Mara nyingi viongozi wa makanisa ya uongo wanatawala kwa nguvu, kwa masharti mengi, kwa kusababisha hofu, na kwa kutisha.*
- Makanisa ya kweli hufundisha mahusiano mazuri ya kimungu katika jamii (1 Wakorintho 5:9–11; 1 Petro 2:11–17). *Makanisa mengine ya uongo yalazimisha kujitoa kutoka jamii ila kwa ajili ya kupata pesa au kuwahubiria watu.*
- Makanisa ya kweli huhimiza upendo na heshima kwa ndugu, ingawa hujua kwamba ndugu akimpuuza Kristo inasababisha kutoelewana (Mathayo 10:34–37; Waefeso 5:22–6:4). *Makanisa ya uongo mengine hulazimisha kufarakana na ndugu wa kimwili wasipoongoka bila kujali maoni ya ndugu kuhusu Kristo.*
- Makanisa ya kweli humkazia Kristo (1 Wakorintho 1:10–17; 2 Wakorintho 4:5–6). *Makanisa ya uongo mara nyingi yamkazia kiongozi au mafundisho ya viongozi tu.*
- Makanisa ya kweli huonyesha heshima kwa watu na taasisi, kama serikali, hata wakiwa watu wapotevu au taasisi za kipotevu zilizoathiriwa na mawazo ya kishetani (Waroma 13:1–7; Tito 3:1; 1 Petro 2:13–17). *Makanisa ya uongo mara nyingi huwahimiza washiriki wake kuwadharau walio nje ya kundi lao.*
- Makanisa ya kweli yana uaminifu na husema ukweli, hata kama italeta madhara kwake (2 Wakorintho 4:2). *Makanisa ya uongo mara nyingi huruhusu chochote kitakacholinda na kusaidia kundi lao.*
- Makanisa ya kweli huwalazimisha viongozi wake waishi maisha adili na kutunza usafi wa kimaadili (1 Timotheo 3:1–13; Tito 1:5–9). *Makanisa ya uongo mara nyingi huwaruhusu viongozi wake kuendelea kuongoza ingawa hawazingatii maisha yanayompendeza Mungu.*
- Makanisa ya kweli hufundisha kwamba utoaji ni kwa hiari (2 Wakorintho 9:7). *Makanisa ya uongo mara nyingi huweka masharti kuhusu utoaji na kudai mali za washiriki zitolewe kwa ajili ya kundi tu.*
- Makanisa ya kweli huwahimiza washiriki wake kupima wenyewe kuona kama wanaongozwa kulingana na Biblia (Waefeso 4:11–16; 1 Yohane 4:1–6). *Makanisa ya uongo mara nyingi huwaambia washiriki wake kwamba hawawezi kujiamulia kuhusu imani au mwelekeo wa kanisa.*
- Makanisa ya kweli huwatambua kuwa Wakristo wote wanaokiri jina la Kristo katika imani yao na mienendo yao (1 Wakorintho 3:1–9; Wafilipi 1:15–18; 2 Yohane 7–11). *Makanisa ya uongo mara nyingi huwatambua watu wa ushirika wao tu.*

# Tofauti Zilizopo kati ya Makanisa ya Kweli na Makanisa ya Uongo

- Makanisa ya kweli hufundisha kanuni za kibiblia ambazo zinawahimiza washiriki kukua kiroho katika akili zao, maamuzi yao, na msimamo wao (2 Timotheo 3:16–17; 2 Yohane 7–11). *Makanisa ya uongo mara nyingi huwafanya washiriki wake kuwa na utegemezi wakimwangalia kiongozi tu kuwaamulia vyote.*
- Makanisa ya kweli huepukana na mitindo ya ujanja ya kuwavuta watu, yakiuamini uwezo wa Roho wa Mungu kufanya kazi katika maisha ya watu kupitia Neno la Mungu (1 Wakorintho 2:3–5; 2 Wakorintho 2:17; 10:1–6). *Makanisa ya uongo mara nyingi huitumia mitindo mikali ya kuwavuta na kuwabana watu wasitoke kundi lao, na mitindo mingine ambayo inafanana na ya wafungwa wa gerezani.*
- Makanisa ya kweli hupendwa au huchukiwa kwa sababu ya kujitambulisha kuwa kwa upande wa Kristo na Neno lake (Mathayo 5:11; Yohane 15:18–21). *Makanisa ya uongo mara nyingi hupendwa au kuchukiwa kwa sababu ya kuongeza kitu au kupunguza kitu katika Kristo na Neno lake.*

## Jipime na Fikira Zako!

Ingawa sisi sote tunapaswa kutambua kuwa tuna mawazo yaliyo hatari akilini mwetu, lakini kuna mawazo na hisia vinavyoibuka mara kwa mara kwa watu ambao wamekuwa sehemu ya makanisa ya uongo. Mawazo hayo ni pamoja na:

- Kuwa na utegemezi kwa viongozi wenye vipaji ambao kwa kujidai kusema kwa niaba ya Mungu wanajifanya kuwa juu ya kukosolewa.
- Kuwa na hisia kali zisizo na mwelekeo dhidi ya makosa na unafiki vya makanisa mengine.
- Kuwa na mawazo ya kujitenga na jamii, kuamini kwamba ni "sisi tu" ambao tunampendeza Mungu.
- Kukata mawasiliano na vyanzo vya habari za nje na kutokuwa na maarifa au kuwajibika kwa nje.
- Mtazamo kuhusu ukweli unabadilika kutoka kuzingatia ukweli mpaka kusema na kuamini kinacholisaidia kundi tu, kikiwa kweli au la.
- Kuwa na mtazamo wa kujivunia unaotegemea imani ya kwamba walio nje ya kundi wametawaliwa na Shetani.
- Kupotea uhuru wakati mawazo ya kibinafsi, hisia za kibinafsi, na maamuzi ya kibinafsi vinabadilishwa kuwa mawazo, hisia na maamuzi ya kundi tu.
- Kuchomwa kwa dhamiri, kundi na kiongozi wake wakiwa wanamshawishi mtu kufanya mambo machafu (hasa ya kujamiiana) yanayovunja ujasiri wa kimaadili.
- Kubadilika kwa matarajio kutoka yaliyoahidiwa mpaka yaliyopokelewa.
- Hofu ya kuondoka kwenye kundi kwa sababu ya kutishwa na wazo la kupoteza uhai wa milele na kukosa tuzo kutoka kwa Mungu.

Haya yameandaliwa kutokana na "How to Identify a Dangerous Religious Group" (RBC Ministries, 2002)



AC|FAR

Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA

www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

# Nani ana Imani?



Kwanza, Mungu hana imani. Biblia haisemi popote kwamba Mungu ana imani. Imani ni kumtegemea mwingine au kutegemea kingine. Kweli kwa lugha moja tungeweza kutumia neno "imani" tukimzungumzia Mungu tukimaanisha kwamba Mungu anajiamini (au anajitegemea) na uwezo wake na hekima mwenyewe. Mungu hujua anachofanya!

Lakini hilo si wanalomaanisha walimu wa Neno la Imani (au Neno-Imani) wakitumia neno "imani." Kama wanavyolitumia neno hili, imani ni nguvu fulani ambayo inafanya kazi kulingana na sheria za kiroho zisizobadilika. Inafanya kazi kupitia maneno yatamkwayo ili anachotaka mtu mwenye kuamini na kusema akipate. Kwa mujibu wa walimu wa Neno la Imani, nguvu hiyo iliyo imani ni kitu alicho nacho Mungu na tunaweza kuwa nacho pia. **Lakini Biblia haisemi chochote kinacholeta maana hiyo.**

---

Halafu, lazima tusisitize kwamba *Wakristo wana imani inayookoa, lakini si wote wanayo imani ya kimiujiza*. Imani ndiyo zawadi kutoka kwa Mungu, kama walivyo sahihi kufundisha walimu wa Neno la Imani (Waroma 12:3; Waefeso 2:8). Lakini, Mungu hajampa kila Mkristo "imani inayong'oa milima." Paulo anaorodhesha imani hiyo kati ya vipaji vya kiroho (1 Wakorintho 12:9; 13:2; taz. Waroma 12:3, 6), na anasisitiza aweke wazi kwamba Wakristo wote hawana vipaji vya aina moja (Waroma 12:4–6; 1 Wakorintho 12:4–6, 14–19, 29–30).

Wakati Yesu alisema kuhusu imani inayoweza kung'oa milima (Mathayo 21:21; Marko 11:23), hakuwa na maana ya kwamba mtu yeyote angeweza kuwa na imani ya aina hiyo. Hoja yake ilikuwa kwamba mtu yeyote *aliye na imani ya aina hii* angepata alichoamini. Lakini imani ya aina hii inatoka kwa Mungu tu na kwa kadiri anavyokusudia (1 Wakorintho 12:12). Nakubali kwamba mara zingine Mungu anampa Mkristo uhakika wa kimungu wa kwamba anakusudia kufanya kitu kilicho kigumu kwa binadamu kuamini. Lakini Yesu hakusema kwamba Mungu angefanya hivyo kwa kila Mkristo au kwamba ingekuwa kitu cha kawaida katika maisha ya kila Mkristo.

Mwishowe, ili kuweka wazi, ni bora kusema wasio Wakristo hawana imani. Kila wakati, Maandiko huwaita wasio Wakristo kuwa

wale *wasio na imani*. Imani si kitu walicho nacho wote, lakini wengine wanashidwa kukitumia; hapana. Imani ni kumtegemea Yesu Kristo kama Mwokozi na Bwana kunakotolewa na Mungu mwenyewe.

## Imani ni Nini?

Hakuna sehemu yoyote katika Maandiko inayoita imani kuwa "nguvu" fulani. Wazo la walimu wa Neno la Imani la kwamba, kwa kutumia imani, wanadamu wanaweza kufanya kisicho kiwepo, au kufanya kisichoonekana kionekane, linapinga Maandiko. Nionyeshe utata uliopo kwa kutumia aya mbili ambazo walimu wa Neno la Imani wanazitumia kujaribu kuthibitisha mawazo yao kuhusu imani.

Walimu wa Neno la Imani mara nyingi hurejea Waroma 4:17 na kudai kwamba Wakristo wanapaswa kumwiga Mungu na neno lake la kuumba (yaani, kwa kuwa Mungu alinena, yote yakawepo, hata sisi tunapaswa kunena ili tunachotaka kiwepo). Lakini aya yenyewe inamtaja Mungu kuwa wa pekee kuweza kufanya kitu kisichopo kiwepo (Waroma 4:17). Paulo anasema wazi kwamba Abrahamu alimwamini Mungu kwa sababu ni Mungu tu (na si Abrahamu) ambaye anaweza kuwapa wafu uhai na kufanya kisichopo kiwepo. Ni Mungu aliyeahidi, na ni Mungu tu anayeweza kutimiza (m. 20–21).

Mara zingine, Waefeso 1:3 inarejewa kujaribu kuthibitisha kwamba Wakristo wana afya njema na mafanikio ambavyo vinawangojea ingawa ni vya kiroho na havionekani, lakini ni kwa kunena kwa imani tu ambako kunahitajika ili vionekane. Mfano huu wa kufasiri Maandiko ni mbaya zaidi kuliko ule wa kwanza. Baraka za kiroho ambazo Paulo anasema tunazo kwa kuungana na Kristo (Waefeso 1:3) ni kufanywa watoto wa Mungu (m. 5), kupata ukombozi na msamaha (m. 7), na ujuzi wa mapenzi yake Mungu (m. 9), kuwa warithi (m. 11), na kuwa na Roho akaaye ndani yetu (m. 13). Baraka hizi si za afya njema au za mafanikio ya kifedha zinazongojea kuonekana kwa nguvu ya imani.

Sehemu ya mafundisho ya Neno la Imani inayotaabisha na ambayo inao uwezo zaidi wa kuangamiza ni fundisho la kwamba imani ya kweli hupinga uhalisia wa mambo vile yalivyo. Kuna punje ya ukweli katika wanachofundisha walimu hao. Tunapaswa kumwamini Mungu bila kusita. Lakini, imani ya kweli haipuuzi hali ya mazingira iliyopo kwamba tukatae kilichopo si kweli au si halisi. Badala yake, imani ya kweli hairuhusu hali ya mazingira yaliyopo kutikisa uhakika tulio nao katika uwezo wa Mungu kufanya alichoahidi.

Fikiria tena mafundisho ya Paulo kuhusu Abrahamu katika Waroma 4. Abrahamu hakukana au kupuuza ukweli wa kwamba mwili wake ulikuwa umezeeka kiasi cha kutokuweza kuzaa mtoto. Abrahamu




Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

hakukiri kwamba, licha ya muonekano na hisia zake, alikuwa bado mzima na mwenye uwezo wa kuzaa! Bali, alikiri kwamba Mungu anaweza kumuwezesha kupata mtoto kupitia mwili wake, ingawa ulikuwa kama umeshakufa (Waroma 4:19).

Walimu wa Neno la Imani hupenda sana kukariri msemo wa Paulo wa kwamba "Tunatazamia kwa makini si vinavyoonekana, bali visivyoonekana" (2 Wakorintho 4:18a). Lakini, kufasiri maneno ya Paulo hapa kuwa uthibitisho wa kukana uhalisia wa hali ya mazingira ni kukosea kabisa. Ni kuchukua msemo kwa makusudi na kupuuza maana yake katika mazingira ya aya. Paulo anaendelea moja kwa moja kusema kwa sababu gani alitazamia visivyoonekana na si vinavyoonekana: "Maana vinavyoonekana ni vya muda tu; lakini vile visivyoonekana ni vya milele" (m. 18b). Wakati Paulo anasema kwamba hakutazamia vinavyoonekana, ni wazi kwamba anatumia lugha ya picha—kwani mtu hawezi kuona kitu asipokiangalia!



Maana yake Paulo ni kwamba haishi maisha yake kulingana na anavyoweza kuona tu, au hauruhusu wasiwasi kuhusu mambo ya muda kumshawishi asahau kutimiza aliyoitiwa na Mungu. Si kwamba anavikana vinavyoonekana na vya muda, hapana. Anavitambua wazi. Angalia msemo wake mistari miwili kabla wa kwamba "maumbile yetu ya nje yanaoza" (m. 16). Msemo huu ni ule wanaoita walimu wa Neno la Imani "negative confession" au "ukiri hasi"; Ni kutamka wazi kwamba mwili unaoza na kuharibika. Kulingana na mfano wake Paulo, tunajifunza hakuna shida tukiongea hivyo, tofauti na mafundisho ya walimu wa Neno la Imani.

Kwa hiyo, kuishi kwa imani na si kwa kuona (2 Wakorintho 5:7), hakuna maana ya kukana uhalisia wa tunavyoviona. Bali, ni kuamini kweli kwamba Mungu atawabariki kwa milele wanaomwamini na atawahukumu kwa milele wale wasiomwamini, na ni kuendelea kuamini hivi ingawa maisha ya sasa si kama tunavyoyataka. Ni kuishi na uhakika kulingana na ukweli wa kwamba Mungu atatimiza ahadi yake ya kutupa sisi katika ufufuo uhai usiofifia na wenye utukufu (m. 1–8).

Ni kosa pia kudai kwamba imani inapinga akili zetu. Imani si kinyume cha akili kamwe, kwa sababu ni mtazamo wa kumtegemea Mungu kwa hakika aliyeumba kila kitu na anayetawala dunia kwa ukweli. Imani hukataa kuyategemea tu yale ambayo akili zetu zinaweza kuyagundua. Methali 3:5 husema "usitegemee akili zako mwenyewe," lakini maana yake *si* kwamba tunapaswa kutotumia akili zetu. Maana yake ni kwamba usiishi kama unajitegemea na unaweza kuongoza maisha yako mwenyewe bila hekima ya kumjua na kumcha Mungu (linganisha m. 6–7).

Haya yameandaliwa kutokana na *The Word-Faith Controversy* (unabridged edition) na Robert M. Bowman, Jr.

# Wahubiri wa Neno la Imani na Biblia


Hapa kuna aya tatu za Maandiko ambazo wahubiri wa Neno la Imani hujaribu kutumia kuthibitisha mafundisho ya kwamba afya njema na utajiri ni vya hakika kwa watu wa Mungu wakinena maneno ya imani.

## "Uishi kwa Muda Mrefu na Kufanikiwa"

(3 Yohane 2)

Aya inayofahamika sana ni ile ya maombi ya Yohane kwa rafiki yake Gayo, maombi ya kumtakia "mafanikio mema ya kila aina" na "afya njema ya mwili kama ulivyo nayo rohoni" (3 Yohane 2). Hakuna shida kabisa tukiwaombea watu wawe na mafanikio na afya njema. Lakini lazima tutambue kwamba Yohane hajasema hakika maombi yake yatajibiwa moja kwa moja. Kumbuka, Yohane anamwombea mwingine, si kujiombea. Hata tukijaribu kutumia mantiki ya walimu wa Neno la Imani hapa, ni vigumu kuona kwa namna gani maombi ya Yohane yanamhakikishia Gayo afya njema na utajiri.

Aidha, kuona kwamba Yohane aliomba kwa namna hiyo, kunaonyesha aliamini mafanikio ya Gayo yalikuwa juu yake Mungu, na si juu ya Gayo! Yohane hakumwambia Gayo kudai afya njema yake na mafanikio.



## "Baraka ya Mara Mia"

(Marko 10:29–30)

Aya inayotumika sana na walimu wanaosisitiza mafanikio ya kifedha ni Marko 10:29–30. Katika aya ile Yesu aliwaambia wanafunzi wake:

> Kweli nawaambieni, kila mtu aliyeacha nyumba, au ndugu, au dada, au mama, au baba, au watoto au mashamba kwa ajili ya yangu na kwa ajili ya Habari Njema, atapokea mara mia zaidi wakati huu wa sasa: nyumba, ndugu, dada, mama, watoto na mashamba pamoja na mateso; na katika wakati ujao atapokea uhai wa milele.

Hakika Yesu hakumaanisha kwamba ukiacha nyumba yako kwa ajili ya kumfuata ungepokea nyumba mia kikwelikweli; au kama mtu yule angemwacha mama yake amfuate Yesu, angepokea mamama mia! Anachosema Yesu ni kitu kama hiki: Ikihitajika uache mali yako au ndugu zako wa kimwili umfuate Kristo (kama ilivyokuwa kwa mitume na mara zingine kwa wafuasi wake siku hizi), utajikuta



Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.

ACFAR

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA

www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

ukiwa sehemu ya "familia" kubwa zaidi. Familia hiyo ni kanisa, ambalo watu wake watakuwa ndugu, dada, mamama, mababa, na watoto, na watakufungulia nyumba zao na kukulisha kutoka kwa mashamba yao. Ndivyo ilivyo kwa wainjilisti na wamishonari kupitia karne zote.

## Mungu ni Mponyaji

(Zaburi 103:2–3; 107:20)

Sasa, tufikirie aya mbili kutoka Zaburi. Katika Zaburi 103:2–3 Daudi anajikumbusha kwamba ni Mungu anayesamehe dhambi zake zote na anayeponya magonjwa yote. Si dhahiri kwamba neno hili ni ahadi ya kwamba Mungu ataponya magonjwa yote ya waumini wote kwa nyakati zote. Katika mstari unaofuata Daudi anajikumbusha kwamba Mungu "ndiye aniokoaye kutoka kifo" (m. 4), lakini hakika msemo huu si ahadi ya kwamba Mungu atamfanya Daudi asife. Tena, mwishowe Mungu "atawaponya" waumini wote wasiwe na ugonjwa au ulemavu wowote kwa kuwafufua kutoka wafu wawe na miili mikamilifu. Lakini kwa wakati unaobaki, kila kupona kwetu, kwa njia za kawaida au za kimiujiza, ni baraka kutoka kwa Mungu.

Katika Zaburi 107:20, hoja nyingine tofauti inatolewa. Mtunga Zaburi anawazungumzia wanaume walioasi dhidi ya Mungu, "wakateseka kwa sababu ya uovu wao," na kwa sababu hiyo, wakawa karibu kufa. Walimlilia Mungu, akawaokoa kutoka katika kifo kisicho cha wakati uliofaa (v. 19). Hapa hakuna ahadi ya kila wakati kwa kila mtu isiyotegemea mazingira yake.

## Uvumilivu wa Ayubu

(Yakobo 5:10–11)

Kauli ya Neno la Imani ya kudai kwamba watu wanaoishi kwa imani wanaweza kupata taabu au kuteseka lakini hawapati magonjwa haiandamani na mfano wa Ayubu. Sehemu kubwa ya kuteseka kwake kulikuwa magonjwa yake (m. 10–11). Walimu wengi wa Neno la Imani hudai Ayubu alikuwa mfano wa kutoamini, lakini Yakobo hakubaliani nao. Badala yake, Ayubu ni mfano wa uvumilivu (m. 11) unaoakisia *imani ya kweli* (linganisha na Yakobo 1:3–4).

Baada ya Ayubu kusema, "Mwenyezi-Mungu amenipa, Mwenyezi-Mungu amechukua," na "Tukipokea mema kutoka kwa Mungu, kwa nini tukatae kupokea pia mabaya kutoka kwake?" tunaambiwa kwamba Ayubu *hakutamka neno lolote la kumkosea* Mungu (Ayubu 1:21–22; 2:10). Kudai kwamba Ayubu alijisababishia taabu zake kwa sababu ya kutokuwa na fikira chanya hakuko sahili.

Ni kweli kwamba *baada* ya rafiki zake kujaribu kueleza sababu ya kuteseka kwake, Ayubu alianza kujitegemea na kujivunia, akahitaji kutubu (40:3–5; 42:1–6). Lakini, Mungu aliwaambia rafiki za Ayubu kwamba hawakumsemea Mungu sahihi, kama alivyotamka Ayubu (42:7). Kwani, rafiki za Ayubu walidai kwamba Ayubu alijisababishia mateso yake kwa sababu ya dhambi, tena dhana ile ya walimu wa Neno la Imani imeonekana kuwa uongo.

Haya yameandaliwa kutokana na *The Word-Faith Controversy* (unabridged edition) na Robert M. Bowman, Jr.

# Methali kuhusu Fedha

| | |
|---|---|
| **Hongo** | Anayetamani faida ya ulanguzi anaitaabisha jamaa yake, lakini achukiaye hongo ataishi.—*METHALI 15:27*<br>Mtu mbaya hupokea hongo kwa siri ili apate kupotosha haki.—*METHALI 17:23* |
| **Madeni** | Usiwe mmoja wao wenye kuweka ahadi, watu ambao hujiweka wadhamini wa madeni. Ikiwa huna chochote cha kulipa, hata kitanda unacholalia kitachukuliwa! —*METHALI 22:26–27*<br>Tajiri humtawala maskini; mkopaji ni mtumwa wa mkopeshaji.—*METHALI 22:7* |
| **Bidii** | Uvivu husababisha umaskini, lakini mkono wa mtu wa bidii hutajirisha. Mwenye busara hukusanya wakati wa mavuno, kulala wakati wa kuvuna ni aibu.—*METHALI 10:4–5* |
| **Tamaa** | Amani rohoni humpa mtu afya, lakini tamaa huozesha mifupa.—*METHALI 14:30* |
| **Udanganyifu** | Chakula kipatikanacho kwa udanganyifu ni kitamu, lakini baadaye huwa kama mchanga kinywani.—*METHALI 20:17* |
| **Ukarimu** | Anayemsaidia maskini anamkopesha Mwenyezi-Mungu; Mwenyezi-Mungu atamlipa kwa tendo lake jema.—*METHALI 19:17*<br>Mtu mkarimu atabarikiwa, maana chakula chake humgawia maskini.—*METHALI 22:9* |
| **Uchoyo/ Unyimaji** | Watu humlaani afichaye nafaka, lakini humtakia baraka mwenye kuiuza. —*METHALI 11:26* |
| **Kufanya Biashara kwa Haki** | Faida anayopata mwovu ni ya uongo, lakini atendaye mema hakika atapata faida ya kweli.—*METHALI 11:18*<br>Mali ipatikanayo kwa udanganyifu, ni mvuke upitao na mtego wa kifo.—*METHALI 21:6* |
| **Nidhamu** | Ikiwa unayo hekima ya kutosha, usijitaabishe kutafuta utajiri.—*METHALI 23:4* |
| **Uvumilivu** | Mali ya harakaharaka hutoweka, lakini akusanyaye kidogokidogo ataiongeza. —*METHALI 13:11* |
| **Sifa** | Afadhali kuwa na sifa nzuri kuliko mali nyingi.—*METHALI 22:11* |
| **Ubahili** | Mtu bahili hukimbilia mali, wala hajui kwamba ufukara utamjia.—*METHALI 28:22* |
| **Mafanikio** | Ukinyenyekea na kumcha Mwenyezi-Mungu, utapata tuzo: fanaka, heshima na uhai. —*METHALI 22:4*<br>Anayetegemea mali zake ataanguka, lakini mwadilifu atastawi kama jani bichi. —*METHALI 11:28* |
| **Utajiri wa Kweli** | Kupata hekima ni bora kuliko dhahabu; kupata akili ni chaguo bora kuliko fedha. —*METHALI 16:16* |
| **Kazi** | Mkulima mwenye bidii ana chakula tele, lakini afuataye mambo yasiyofaa hana akili. —*METHALI 12:11* |

Haya yameandaliwa kutokana na *What the Bible Says About Money* na Jessica Curiel (Rose Publishing, 2009)

AC|FAR

Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

# Mtegemee Mungu, Usitegemee Fedha

Ahadi za uongo za fedha zinapita, na mwishowe haziridhishi. Ahadi za Mungu ni za milele na za kuaminika daima.



| Ahadi za Uongo za Fedha | Ahadi za Biblia |
|---|---|
| **Usalama** | Waamuru watu walio matajiri katika mambo ya maisha ya sasa, wasijivune, wasiweke tumaini lao katika mali isiyoweza kutegemewa; bali wamtegemee Mungu, ambaye kwa ukarimu hutupatia vitu vyote tuvifurahie. —1 TIMOTHEO 6:17 |
| **Uwezo na Nguvu** | Basi, usiogope, mimi nipo pamoja nawe. Usifadhaike, mimi ni Mungu wako. Nitakuimarisha na kukusaidia; nitakulinda kwa mkono wangu wa ushindi .... Mimi ndimi Mwenyezi-Mungu, Mungu wako, ndimi ninayetegemeza mkono wako. Mimi ndimi ninayekuambia: 'Usiogope, nitakusaidia." —ISAYA 41:10,13 |
| **Heshima na Hadhi ya Juu** | Watu watakuja kutoka mashariki na magharibi, kutoka kaskazini na kusini na kukaa kwenye karamu katika ufalme wa Mungu. Naam, wale walio wa mwisho watakuwa wa kwanza; na wale walio wa kwanza watakuwa wa mwisho." —LUKA 13:29–30 |
| **Mafanikio** | "Ndugu zangu wapenzi, sikilizeni! Mungu amechagua watu ambao ni maskini katika ulimwengu huu ili wapate kuwa matajiri katika imani na kupokea ufalme aliowaahidia wale wanaompenda." —YAKOBO 2:5 |
| **Kupendwa na Watu** | "Mwenyezi-Mungu, Mungu wako yu pamoja nawe yeye ni shujaa anayekuletea ushindi. Yeye atakufurahia kwa furaha kuu, kwa upendo wake atakujalia uhai mpya. Atakufurahia kwa wimbo wa sauti kubwa." —SEFANIA 3:17 |
| **Amani na Utulivu Moyoni** | "Njoni kwangu nyinyi nyote msumbukao na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha." —MATHAYO 11:28 |
| **Uhuru kutoka kwa Hukumu** | "Utajiri haufai kitu siku ya ghadhabu, lakini uadilifu huokoa kutoka kifo." —METHALI 11:4 |
| **Furaha** | "Uitafute furaha yako kwa Mwenyezi-Mungu, naye atakujalia unayotamani moyoni." —ZABURI 37:4 |



"Msiwe watu wa kupenda fedha; toshekeni na vile vitu mlivyo navyo. Mungu mwenyewe amesema:
Sitakuacha kamwe,
wala sitakutupa."

WAEBRANIA 13:5

Haya yameandaliwa kutokana na *What the Bible Says About Money* na Jessica Curiel (Rose Publishing, 2009)

# Unavyopaswa Kufanya na Fedha na Usivyopaswa Kufanya



| USIFANYE | FANYA |
|---|---|
| Usiipende! *LUKA 16:13* | Mpende Bwana. *KUMBUKUMBU 6:5* |
| Usidhani itadumu. *YEREMIA 17:11* | Mambo ya Mungu tu yatadumu. *MATHAYO 19:21* |
| Usidhani inaweza kukuokoa. *ZABURI 37:16–17* | Kumbuka kwamba Mungu tu anaweza kukuokoa. *ZABURI 27:1* |
| Usiitumikie. *MATHAYO 6:24* | Mtumikie Bwana. *1 PETRO 5:2; MARKO 12:41–44* |
| Usiwaonee wivu wengine walio nayo. *KUTOKA 20:17* | Jiridhishe na vitu ulivyo navyo. *LUKA 3:14* |
| Usiwe mchoyo. *YAKOBO 5:3–6* | Kumbuka kwamba Mungu hujalia. *YOBU 1:20–21; YAKOBO 4:13–15* |
| Usiitumie kipumbavu. *METHALI 17:16* | Itumie kwa hekima. *METHALI 31:10–31* |
| Usidhani kwamba itakufariji wakati wa taabu. *METHALI 15:16–17* | Jipatie amani katika Mungu. *WAROMA 15:13* |
| Usiitegemee. *ZABURI 62:10* | Mtegemee Mungu. *METHALI 18:10–11* |
| Usidhani itakununulia baraka za Mungu. *MATENDO 8:9–24* | Jipatie baraka kwa kuishi kwa Mungu. *2 WAKORINTHO 6:10* |
| Usiitumie kwa udanganyifu. *MIKA 2:2* | Itumie kulipa madeni yako. *ZABURI 37:21* |
| Usiwashinikize wengine ili kuipata. *METHALI 22:16; AMOSI 2:6–7* | Fanya kazi ili kuipata. *2 WATHESALONIKE 3:9–11* |
| Usiibe kuipata. *TITO 2:9–10; KUTOKA 20:15* | Itumie kwa haki. *WALAWI 25:14; ZABURI 112:5* |
| Usiwape heshima maalumu wale walio nayo. *YAKOBO 2:2–6* | Itoe kwa wale wenye taabu. *MATHAYO 5:41–42.* |
| Usiitumie kwa ujanja. *METHALI 13:11* | Uwe mwaminifu ukiitumia. *METHALI 11:1* |
| Usiitumie kwa uovu. *EZEKIELI 8:12–13* | Mheshimu Mungu nayo. *METHALI 3:9–10* |
| Usipokonye mali za watu. *EZEKIELI 22:29* | Fanya bidii uipate. *METHALI 13:4* |
| Usiwe mlafi. *LUKA 12:15* | Itoe kwa kusudi. *1 WAKORINTHO 16:2* |
| Usiwe na wasiwasi juu ya fedha. *MATHAYO 6:34* | Kumbuka kwamba Mungu atakutunza. *METHALI 15:25* |

Haya yameandaliwa kutokana na *What the Bible Says About Money* na Jessica Curiel (Rose Publishing, 2009)

AC|FAR


Tunawatayarisha watu wa Mungu kwa ajili ya kupambanua, kutetea imani, na kufanya uinjilisti kati ya washiriki wa makanisa ya uongo.

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • barua pepe info@ACFAR.org • simu +256782 000 664 • ofisi +256713 000 664

# Ufafanuzi wa Biblia katika Mazingira na Utamaduni wa Kiafrika

*(Africa Bible Commentary)*

*Nairobi: WordAlive Publishers, 2010*
*1,832 kurasa*




Kitabu hiki ni kitabu cha kipekee kuwahi kuchapishwa–kinahusu ufafanuzi wa Biblia katika juzuu moja lililotolewa kwa mara ya kwanza hapa Afrika na wanatheolojia Waafrika ili kuyakidhi mahitaji ya wachungaji wa Kiafrika, wanafunzi na viongozi wa kanisa. Kwa kufasiri na kuzingatia matumizi ya Biblia katika miktadha halisi ya utamaduni wa Kiafrika ulivyo sasa; kitabu hiki kinayaelezea Maandiko Matakatifu vizuri sana na kwa undani kwa njia bora zinazoafiki bara la Afrika kwa umuhimu wake. Kitabu hiki kinatoa ufasiri wa sehemu kwa sehemu ambao unaambatana na muktadha wa Kiafrika unaoeleweka kwa urahisi.

*Note: Na including a work we are not necessarily endorsing of all its contents or of other works na the same author or publisher.*

---

**DINI ZOTE SI SAWA:** Marejeo kutokana na makala ya WINGI WA DINI. *Yameandaliwa na Tokunbo Adeyemo.*

**WAKRISTO WANAWEZA KUDANGANYWA:** Marejeo kutokana na makala ya UASI WA KITHEOLOJIA. *Yameandaliwa na James Nkasah-Obrempong.*

**MAONYO YA MAANDIKO DHIDI YA UCHAWI NA USHIRIKINA:** Marejeo kutokana na makala ya UCHAWI. *Yameandaliwa na Samuel Waje Kunhiyop.*

**JE, TUWATEGEMEE MALAIKA KWA MSAADA WA KIROHO?** Marejeo kutokana na makala ya MALAIKA, PEPO WABAYA NA MAMLAKA. *Yameandaliwa na James Nkasah-Obrempong.*

**NANI ANA IMANI?** Marejeo kutokana na makala ya IMANI NA UTAFUTAJI WA ISHARA. *Yameandikwa na Adama Ouedraogo.*

**MTEGEMEE MUNGU USITEGEMEE FEDHA:** Marejeo kutokana na makala ya MALI NA UMASKINI. *Yameandikwa na Stephen Adei.*

# DAFTARI HILI LISIUZWE

"Tumshukuru Mungu kuna wale katika kanisa la sasa wanaojikita katika kazi ya kulinda na kutetea ukweli wa Mungu uliofunuliwa. Lakini mara zingine wanaweza kukosa upendo….Inaonekana kwamba hawafurahii chochote kingine zaidi kuliko kubishana. Wengine wanafanya kinyume cha kosa hili. Wanajikita katika ya kutunza na kuonyesha upendo wa kindugu, lakini ili wafanye hivyo wako tayari kuachana na kweli za msingi za ufunuo. Mielekeo hii yote miwili haiko sawa wala si ya kibiblia. Ukweli unaweza kuwa mgumu usipolainishwa na upendo; upendo unaweza kuwa dhaifu usipoimarishwa na ukweli. Mtume Paulo anatuita tuyaunganishe mambo haya mawili, kitu ambacho si kigumu kwa waumini waliojazwa na Roho, kwa sababu Roho Mtakatifu mwenyewe ni 'Roho wa ukweli' na tunda lake la kwanza ni 'upendo.' Hakuna njia nyingine tofauti na hii ili tupate umoja wa kikristo uliokomaa."

Yameandaliwa kutokana na *The Message of Ephesians: God's New Society* na John R.W. Stott (InterVarsity, 1991)

Daftari hili limeletwa kwako na


**Africa Centre for Apologetics Research**

Post Office Box 72405
Clocktower, Kampala, UGANDA

**simu** +256782 000 664
**ofisi** +256713 000 664
**barua pepe** info@ACFAR.org
**intaneti** www.ACFAR.org


"Na sala yangu kwa ajili yenu ni kwamba upendo wenu uzidi kuongezeka siku hadi siku pamoja na maarifa na busara ili mpate kutambua mambo yaliyo mema. Na pia mpate kuwa watu safi, wasio na hatia hadi siku ya Kristo. Maisha yenu yawe na matunda ya haki yatokayo kwa Yesu Kristo, ili Mungu apewe utukufu na sifa."

(Wafilipi 1:9–11)

"…basi muishi kama watoto wa nuru. Kwa maana tunda la nuru hupatikana katika kila lililo jema, lililo la haki na la kweli. Jifunzeni mambo yanayompendeza Bwana. Msishiriki matendo ya giza yasiyofaa, bali yafichueni."

(Waefeso 5:8b–10)

"Msiige tabia na mienendo ya dunia hii bali mbadilishwe, nia zenu zikifanywa kuwa mpya, ili mpate kuwa na hakika ni nini mapenzi ya Mungu: yaliyo mema, yanayopendeza machoni pake na makamilifu."

(Waroma 12:2)

REV3 02/15